

MAPAMBANO KATI YA MUNGU NA SHETANI

 Kusikia nyimbo hizi nzuri sana, kulisikia hili kanisa likiziimba, na kuwazia juu ya nyakati za kale, na kuangalia huko na kuona nyuso sijaziona kwa muda mrefu, basi kuna jambo fulani kulihusu, ambalo ni halisi, kurudi kanisani. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vyema. Nilikuwa muda mfupi tu uliopita . . .

² Rafiki wa siku nyingi sijapata kumwona, loo, kumpungia mkono, nadhani, bali imekuwa ni miaka kadha tangu niliposhirikiana naye; mvulana fulani, Jim Poole, nilikuwa nikitembea pamoja naye, nilipokuwa mvulana. Na sasa alikuwa huku chini, nyumbani kwangu, muda mfupi uliopita, mara ya kwanza aliyopata kuwa kwangu tangu tulipokuwa, vema, tangu nilipooa.

³ Naye Bibi Wood hapa alimwalika, kushuka kuja kutusikia tukihubiri. Akasema, “Vema, nilikuwa nikimsikiliza wakati wote.”

⁴ Na wakati tulipokuwa tukitembea pamoja, tukiwinda, na kadhalika, nasi . . . hakuninii . . . Asingesema mengi sana, mwajua. Nilikuwa nikizungumza wakati wote. Nikasema, “Mbona usiseme kitu fulani?”

Akasema, “Ninawezaje?” Nilichukua tu wakati wote.

⁵ Kwa hiyo inaonekana kana kwamba kwa namna fulani imekuwa hivyo kwangu. Kidogo kuchukua wakati, kuzungumza sana, na kuendelea, pasipo kufika popote. Bali ninayo furaha, leo hii, kwamba nimebadilisha njia yangu ya kuzungumza tangu siku hizo, nazungumza juu ya Bwana. Ninampenda sana.

⁶ Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Ruddell, naye alikuwa akiniambia pale . . . (Asante, Ndugu Temple.) Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Ruddell. Naye alishuka akaja siku chache zilizopita, na alikuwa akizungumza nami, na akaniambia ndoto tatu ambazo angeninii . . . alizoota. Nami nikapata mbili za hizo, nikasahau hiyo nyingine. Nilikuwa nikijaribu kumwambia ilikuwa ni nini. Ilikuwa ni mimi nikiwa na kioo, nikijaribu kuakisi, na kusema, “Unaona jinsi Mungu anavyoakisi, kama tu tunavyoakisi katika—katika kioo.” Bila shaka amekuwa mwema.

⁷ Ndugu Creech, huyu ni msichana wako anayecheza piano? Kweli? Sikujua kama huyo alikuwa ni Patty. [Ndugu fulani anasema, “Wako moja kwa moja kule nyuma jukwaani.”—Mh.]

Yuko wapi Patty? Vipi. . . Jamani, salaale! Patty. Ninakumbuka wakati walipoishi kule chini, vema, mumo humo wanamoishi sasa, ni karibu kama jamaa huyu mdogo anayeketi papa hapa. Naye Mary Jo ni, nadhani, ameolewa. Jim alikuwa amesimama pale muda mfupi uliopita. Mjukuu wake alikuwa amesimama pale, na huyu hapa mjukuu wangu akaingia. Nikasema, “Afadhali tuchukue fimbo ya kutembelea kisha tuketi chini. Sivyo?”

⁸ Lakini ng’ambo tu ya Mto, hapo ndipo Mahali pakubwa. Hapo ndipo tunapotazamia. Na si tu kwa sababu nina. . . ninazeeka, kwamba ninawazia Hilo. Nilianza kuzungumzia Hilo nilipokuwa mdogo, jamaa mdogo tu, kijana mdogo kwenye ujana wangu kabisa. Ninaamini kwamba kulikuwako na Nchi mahali fulani. Tunaelekea Huko. Nina furaha sana kwa ajili yake.

⁹ Mwajua, si—sisemi mengi sana yanayofaa kitu, hasa sana wakati unapozungumza tu.

¹⁰ Lakini, mara nyingi ninachukua kitu fulani hapa, kwenye Maandiko. Lakini wakati mwingine Bwana hunipa kitu, nalo linanifurahisha kupindukia ninaposhika kitu ambacho ni kizuri kweli. Ninaninii tu, loo, linanitendea mema sana. Sote tunajisikia hivyo. Ninajua Ndugu Neville, wewe, na ndugu hapa, Ndugu Junior, na nyinyi nyote, mnajisikia vivyo hivyo, unapopata jambo fulani ambalo Bwana anakupa, nawe unaona kwamba ni halisi sana.

¹¹ Na hivi majuzi usiku, nilikuwa nikihubiri, ninaamini ilikuwa ni maskani, nami nikagusa kitu fulani ambacho kimenisaidia sana kuliko chochote nimewahi kuwazia tangu nilipoongoka. Na hicho kilikuwa. . . huenda nikakirudia tena, kama ni sawa. Ninajua ambapo mnajua ninakoelekea, lakini, bali, ilikuwa ni thibitisho la wokovu. Mnaona? Ni. . . Lilinigusa tu, nami ni—nikalisema. Nikaenda nyumbani, nikaingia chumbani mwangu, nami nikatembea huku na huku sakafuni. Ni—nilikuwa tu na wakati mdogo, mzuri peke yangu, mwajua, mle ndani tu nikiliwazia.

¹² Basi mambo yalikuwa hivi. Huenda nikawaelezea tu kwa dakika moja. Nilikuwa nikizungumza kuhusu, “Sisi ni wamiliki wa kitu chote. Kila kitu ni chetu.” Wao wanasema sisi ni wenye kichaa, mwajua. Lakini hata hivyo, iwayo yote, yote ni mali yetu. Mnaona? Mnaona? Na huenda sisi. . . Hiyo ndiyo sababu kidogo tunatenda kipekee, mnaona, sisi ni warithi wa vitu vyote. Mnaona?

¹³ Nami nilikuwa nikiwazia, tunamiliki upendo, furaha, ujasiri. Tunamiliki imani, na uvumilivu, utu wema, saburi, upole. Usingeweza kununua hayo kwa aina yoyote ya pesa. Haijalishi, hakuna. . . Shuka uende ukaninunulie saburi yenye thamani ya robo, unaona. Kamwe usingeweza. Na, hata hivyo, Mungu anatupa hiyo. Tunamiliki hiyo. Hiyo ni mali yetu.

Kisha utununulie imani kidogo. Tungekuwa radhi, kutoa yote tuliyokuwa nayo, kwa ajili ya imani kidogo. Unaona? Lakini, tumepewa hiyo, na kila kitu ni bure, kikitoka kwa Bwana. Hilo si ni la ajabu?

¹⁴ Kisha nikawazia hili: wakati Israeli, wakati mmoja watumwa, watoto wa Mungu katika utumwa, huko Misri. Sasa, huo ulikuwa ni urithi wa Mungu, kama tu tulivyo leo hii. Halafu labda wangewaletea chakula, lundo la mikate iliyonyonyoka, na kutupwa nje, na chochote walichopata. Kumwua mmoja, ni kama tu kumwua mbwa ama chochote kingine. Nao walitamani ukumbozi kutoka kule. Walikuwa wamekaa mle muda wa miaka mia nne.

¹⁵ Ndipo siku moja, akaja nabii, akitoka nyikani kwa kishindo, huku Nu—Nuru ikimfuata. Naye akawaambia, “Kuna nchi iliyojaa maziwa na asali, naye Mungu alikuwa amewapa hiyo.” Naye akafanya ishara na maajabu, kuwaonyesha kwamba yeye hakuwa ni wa bandia, kitu fulani cha uongo, bali kweli alikuwa ameagizwa na Mungu kuwapeleka watu hao kwenye nchi hiyo.

¹⁶ Sasa wazia hilo. Watoto wao, wasimamizi wa watumwa walikuja, kama walitaka kumwua mmoja, hilo lilikuwa ni sawa tu. Hakuna kitu kingaliweza kusemwa. Wanaenda wanamchukua binti yako mdogo, kwa uharibifu mkubwa, mbona, hakuna chochote lingaliweza kusemwa. Ilikubidi kusimama tu pale, na kumwacha aende. Unaona? Mvulana wako, kidogo alipata . . . hakufanya kazi vizuri tu, nao wanataka kumwua kwa sababu ya hilo. Kumwua, hilo ni sawa, hakuna chochote kingaliweza kusemwa.

¹⁷ Lakini sasa wanaambiwa kwamba wanatoka kwenye utumwa huu, nao wanaenda kwenye nchi iliyojaa maziwa na asali, nao wanaweza kuwa na shamba lao wenyewe. Wanaweza kukuza vitu vyao wenyewe, wawalishe watoto wao wenyewe, wawapeleke shuleni, waishi kwa amani. Nayo nchi hiyo kuu, nayo ni mali yao. Mwajua, hiyo ilikuwa ni ahadi kubwa. Wazieni kile hilo lilichomaanisha.

¹⁸ Vema, nabii huyu alifanya miujiza mingi sana miongoni mwao hata wakaona kwamba—kwamba kweli alikuwa ni mtu aliyetumwa na Mungu. Vema, wakatoka, wakaingia huko nyikani.

¹⁹ Ndipo walipofika Kadeshi-barnea, sasa, Kadeshi-barnea ndiyo kiti cha hukumu. Ilikuwa hivyo siku hizo, kwa ulimwengu. Kadeshi-barnea, palikuwa ni mahali penye chemchemi kubwa, na chemchemi nyingi ndogo, vijito vingi vya chemchemi hii.

²⁰ Vema, hapo walikuwa na mtu miongoni mwao, shujaa mashuhuri, jina lake Yoshua. Yoshua ni “Yehova-Mwokozi.” Basi Yoshua aliingia kwenye hiyo nchi ya ahadi.

²¹ Sasa, kumbukeni, hamna mmoja wao aliyepata kuwa kule. Hawakujua kama hiyo nchi kweli ilikuwako ama haikuwako.

Walininii tu, kwa imani, walifuata waliyoambiwa, kwamba Mungu alikuwa na mahali kwa ajili yao. Nao walikuwa wakienda mahali hapo, kwa imani tu. Sasa wazia hilo. Wakaondoka Misri, naye Mungu akawatoa, na sasa wanaikaribia nchi hiyo. Halafu basi wanapoikaribia nchi hiyo, Yoshua anaingia mle nchini na kurudi na thibitisho. Anavuka Yordani, anaingia Palestina, anarudi na ushahidi, kichala kikubwa cha zabibu kilichohitaji watu wawili kubeba. Nao wangeweza kula zabibu hizo. Naye akasema, “Nchi hii iko vile vile hasa Mungu alivyosema ilikuwa.”

²² Loo, huo ulikuwa ni uhuru wa jinsi gani, ambako wangeweza kwenda sasa. Nao wangeweza kuwa na mashamba yao wenyewe, na kuwalea watoto wao. Na kuwa na...na baraka za Mungu juu yao, na kuishi kwa amani. Hakukuwako na mtumwa wa mtu yeyote. Jinsi...Lakini, hatimaye, baada ya kuishi maisha mazuri marefu, hatimaye iliwabidi kufa, hata hivyo wakiwa ni watoto wa Mungu. Iliendelea mwaka baada ya mwaka, wakikuza mazao yao, na kuwa na familia zao, na maisha mazuri ya amani, kisha wanakufa.

²³ Ndipo, siku moja, akashuka Shujaa aliye mkubwa kuliko wote, Bwana Yesu, Mwana wa Mungu. Na Yeye akasema, “Kuna Nchi ambamo mtu hafi. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Kama sivyo, ningaliwaambia. Naenda kuandaa mahali, kisha nirudi kuwapokea.” Sasa, Yeye ni Nabii ajaye, akinena juu ya Nchi iliyo tu ng’ambo ya mto Yordani, mauti. Ambamo, kwamba, ingawa mna mashamba yenu, mna familia zenu, mmebarikiwa na Mungu, lakini hata hivyo hamna budi kufa. Lakini, hata hivyo, kuna Nchi iliyo ng’ambo ya hiyo, ambamo hamfi. Loo, jamani!

²⁴ Ndipo Yeye akaja Kadeshi-barnea, Kalvari, kile kiti cha hukumu, tena. Ambapo, hukumu ya dhambi, iliyowafanya watu kufa, ililipiwa hukumuni, kwenye Kadeshi-barnea Yake. Yeye alilipa deni ya dhambi, akafa; akavuka Yordani, Yordani ya mauti; akafufuka siku ya tatu, akarudi. Naye akasema, “Niguseni, roho hana mwili na mifupa kama nilivyo Mimi. Mna chakula?” A—Akala samaki na mkate. Naye alikuwa pamoja nao siku arobaini, akithitibisha, kama Yoshua, kwamba hiyo Nchi ilikuwako. Yeye Ndiye thibitisho la ile Nchi kule.

²⁵ Sasa, Yeye alisema, “Wote watakaoamini hili, enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa.”

²⁶ Halafu, kwenye Siku ya Pentekoste, Yeye alituma arabuni ya Mahali hapa, lile hakikisho, thibitisho ya kwamba Nchi hii ni halisi. Kama tu vile Yoshua alivyorudi pamoja na lile thibitisho, Yesu alileta thibitisho la Roho Mtakatifu.

²⁷ Sasa, tunajihesabu tumekufa. Tumezikwa pamoja na Yeye katika ubatizo, katika kifo Chake.

²⁸ Nasi tumefufuka pamoja na Yeye, katika ufufuo. Na sasa tuko ndani, tayari, sio kwamba tutakuwa. Tayari tumefufuliwa. Loo, jamani! Sisi sasa, sio tutakuwa, sisi sasa, usiku wa leo, tumeketi katika mahali pa Mbinguni (vipi?) katika Kristo Yesu. Sio tutakuwa, wakati mwingine. Tuko sasa. Kanisa halitambui kwamba wao ni nani. Mnaona? Sisi sasa, dakika ii hii, (jinsi gani?) katika Kristo Yesu, tumekusanyika pamoja ndani Yake, tayari tumefufuliwa kutoka kwa wafu. Nafsi zetu hazingeweza kufa.

²⁹ Sasa hebu tusimame kwa dakika moja. Hapa, wakati mmoja, tulikuwa tukisema uongo, kuiba, kudanganya, kupigana, kulaani, kila kitu kingine. Ndipo basi tukakiri dhambi hiyo yote. Ndipo tukazikwa pamoja na Yeye katika ubatizo, na kufufuliwa pamoja na Yeye. Ndipo tunapofufuka... “Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea lile thibitisho,” thibitisho la Nchi hii nzuri. Ndipo Roho huyo anayekuja juu yetu, hutuinua kutoka kwenye huo udanganyifu, kuiba, na upuuzi huo wote huko nyuma, na sasa tumefufuka pamoja na Yeye, sasa tumeketi pamoja na Yeye, *hapa* juu katika mahali pa Mbinguni. Nafsi zetu zote ziko tayari kabisa.

³⁰ Mbona, William Branham amekuwa amekufa kwa miaka thelathini na kitu. Nilifanyika kiumbe kipya. Mtu huyo wa kale alikufa. Niliangalia nyuma kule, nikizungumza na yule rafiki yangu, alasiri ya leo, akasema, “Unakumbuka tulipokuwa tukifanya *hivi na hivi*? Kumbuka tulimtupa yule mvulana majini usiku huo, akikoroma.”

Nikasema, “Naam. Nisingefanya hivyo tena.” Mnaona?

³¹ “Unakumbuka wakati ule tulipokuwa tukitaka kuichomelea pini ile kwenye yule chura, wakati alikuwa ‘gruu’ namna hiyo, na *hivyo*?”

“Naam,” nikasema, “nakumbuka hilo.”

³² Na mambo haya yote tuliyofanya! Nikawaza, “Unajua, hiyo ni wakati nilipokuwa—hiyo ni wakati nilipokuwa... Hiyo ni wakati nilipokuwa nimekufa. Mnaona? Lakini sasa mimi ni hai.” Mnaona? Loo, sifanyi hayo sasa.

³³ Tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, na sasa tuna arabuni ya wokovu wetu, malipo ya kwanza. Kitu hicho kinagharimu dola elfu kumi, na Yeye akatupatia elfu moja ya kwanza. Mnaona? Hii ndiyo sehemu ya kumi ya kwanza, ya arabuni yetu. Ambapo, tayari tumefufuka kutoka dhambini na kutokuamini, tukaingia katika ufufuo pamoja na Kristo. Na sasa tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, pamoja na thibitisho hilo, kama lile Yoshua alilorudi nalo. Hiyo Nchi iko Kule, nasi tuko njiani mwetu. Hakuna mauti tena. Hatuwezi kufa.

³⁴ Wanakwambia, wakati mwingine, “Ndugu Branham alikufa,” kamwe usiamini hilo. Kwa nini? Ndugu Branham hawezi kufa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Siwezi kufa; nimekufa tayari. Sasa, William Branham alikufa, muda mrefu uliopita, yapata miaka thelathini iliyopita, ama zaidi, yapata miaka thelathini na miwili iliyopita. Nimekuwa nikihubri yapata miaka thelathini na miwili, kwa hiyo yeye alikufa hata kabla ya hapo. Lakini, sasa, hiki ni kiumbe kipya.

³⁵ Russell Creech, kiumbe kipya. Yeye siye yule mvulana mdogo, aliyekuwa akikimbia huko chini, chini ya Corydon. Orman Neville siye yule mvulana mdogo aliyekuwa. Na—na Ndugu Ruddell si maskini mvulana yule mdogo aliyekuwa, mwajua. Na—na Ndugu Jackson, hawa wengine wote, sio jamaa hao. Nyinyi nyote ndugu na dada, sisi sio hao watu tuliokuwa. Sisi ni—si ni viumbe vipya, uumbaji mpya. Haikubidi kulihofia. Tayari tupo *hapa* juu. Angalieni mahali tulipokuwa. Angalieni mahali tulipo sasa. “Viumbe vipya katika Kristo Yesu.” Loo, jamani!

³⁶ Sasa, unajua, Russell, ninajisikia kana kwamba karibu ningeumba ule wimbo, ambao, kila ninapousikia, ninakufikiria wewe na Dada Creech.

Nitaruka niende, Ee utukufu,
Nitaruka asubuhi.

Naam, bwana! Mnakumbuka tulizoea kuuimba huo?

Nitakapokufa, haleluya, hivi karibuni,
Nitaruka niende.

³⁷ Ninaupenda huo. Nasi tunapoanza kuzeeka, nazo nywele zinaingia mvi, mabega yanainama, hilo linamaanisha mengi kwetu kuliko wakati wowote. Mnaona? Kwa sababu, mtoto hutazamia mbele: atamwoa nani, atawaelimishaje watoto wake? Na hayo yote yamekwisha, ndipo wakati huo karibu wewe umekwisha, unaona, ndipo unakukabili kutua kwa jua.

³⁸ Lakini wazia tu, ndugu, hakuna kitu ila tulicho nacho. Tunao upendo. Tunayo furaha. Tunayo amani. Tunao Uzima. Tunayo... Tunamiliki mauti. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema tunayamiliki. Tunamiliki mauti. Ni mali yetu. Sisi si mali yake; hayo ni mali yetu.

Wasema, “Utafanya nini na mauti?”

Kama tu vile Paulo alivyosema, wakati alipokuja akibisha mlangoni. Kasema, “Umekuja kunisindikiza kuuvuka ule Mto?”

³⁹ Naye mwandishi wakati mmoja alisema, “Mungu aliyafunga mauti kwenye kigari, na jambo pekee yanayoweza kufanya ni kukuvuta Mbele za Mungu.” Hivyo tu. Huwezi kufa. Waliyafungia tu mauti kwenye kigari, na jambo pekee yanayoweza kufanya ni kukuvuruta moja kwa moja juu hadi Uweponi mwa Mungu. Ni kileta bahati, cha kuja

kukuvusha Mtoni. Hivyo tu ndivyo yalivyo. Kwa hiyo hakuna kitu kinachoweza kutusumbua, tena.

⁴⁰ Paulo alisema, wakati mauti yalipokuja yakifingirika kuupitia huu, ule wakati wake, alisema, “Ee mauti, uko wapi mwiba wako?”

Kasema, “Vema, nitakupeleka kaburini.”

⁴¹ Akasema, “Basi, kaburi, uko wapi ushindi wako? Ninakumiliki, pia.” Ndipo akageuka, kasema, “Ashukuriwe Mungu Yule atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

Basi, tunao, Ndugu Temple. Jambo ndilo hilo. Imekwisha.

⁴² Vema, Dada Snelling alizoea kuimba wimbo wa kale. Sidhani yeyote wenu labda anamkumbuka Dada Snelling. Nilikuwa kwenye kaburi lake hivi majuzi. Alikuwa akiimba yubile ndogo ya kipentekoste, kuhusu:

Hebu twendeleeni, hebu twendeleeni,
Kuzungumza juu ya Njia hii nzuri ya
kale;
Hebu twendeleeni, hebu twendeleeni,
Kuzungumza juu ya Bwana.

Mlipata kuusikia?

Ninajisikia vizuri zaidi, kuzungumza tu
kuhusu Njia hii nzuri ya kale,
Ninajisikia vizuri zaidi, ninazungumza juu ya
Bwana.

⁴³ Jambo ndilo hilo. Vema. Hebu tuzungumze na Yeye kwa dakika moja sasa, katika maombi, kabla hatujaanza, kulisoma Neno Lake.

⁴⁴ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, na macho yetu yamefungwa, na masumbuko ya siku yakipita sasa. Tumekusanyika katika Jina Lake, na katika Uwepo Wake. Huenda kuna watu hapa wanaweza kukumbuka jambo fulani ungetaka likumbukwe mbele za Mungu? Inua tu mkono wako, na kwa huo, “Mungu, nikumbuke tu.”

⁴⁵ Baba yetu wa Mbinguni, Mungu asiye na kikomo Ambaye alijua, kabla ulimwengu haujapata kuumbwa, kwamba tungekuwa tumesimama hapa usiku wa leo. Umeiona mikono hiyo. Unajua kilicho nyuma ya kila mmoja wayo, kile kilichokuwa chini ya huo moyo ambao mkono huo ulinuliwa juu yake. Ninawaombea, Baba, kwamba Wewe utajibu kulingana na utajiri Wako mkuu katika Utukufu na Nguvu Zako.

⁴⁶ Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya mchungaji wake, halmashauri yake, wadhamini wake, mashemasi, washiriki wote, na kwa ajili ya watu hao wote wa thamani wanaokaa kwa muda hapa Clarksville, wasafiri, wageni, si wa ulimwengu tena. Walisalimisha kila kitu cha

ulimwengu, wakauza yote waliyokuwa nayo, na kununua Lulu hii ya thamani kuu, Bwana Yesu Yeye atupaye Uzima wa Milele. Tunakushukuru Wewe kwa ajili Yake, Bwana. Asante kwa ajili ya nafsi hizi za thamani. Ninamwombea kila mmoja.

⁴⁷ Ninawazia juu ya Ndugu Jackson, na jinsi ambavyo amefanya kazi sana na kujaribu, kujitahidi sana, akijaribu kuwalisha kondoo, na kufanya mahali pa wasafiri kukutanika, kuwaweka pamoja, tukikungojea Kuja kwa Bwana; yeye pamoja na mke wake, na familia. Huku wameketi hapa nyuma yangu, usiku wa leo, Ndugu Ruddell, naye pia anawaweka pamoja, kundi dogo linalokaa kwa muda kwenye 62. Ndugu Neville, na lile kundi huko maskanini, linalokaa kwa muda. Na wengine, Bwana, waliopo, huenda wakawa hapa kutoka mahali pengine. Tunakutazamia Kuja kwa Bwana.

⁴⁸ Tusamehe, Bwana, tunapokusanyika sasa pamoja. Tunakuja katika Jina la Yesu, tukijua ya kwamba Wewe uliahidi kutusikia. “Lolote tungeomba katika Jina Lake lingejaliwa.”

⁴⁹ Na sasa, usiku wa leo, tunapoifungua Biblia, kuingia kwenye somo dogo, sasa, hatupo hapa tupate kuonekana au kusikika, kama tu wanadamu. Hao watu hawaketi katika chumba hiki, kusema tu, “Vema, nilihudhuria kanisa usiku wa leo.” Tunatarajia kutembelewa na Wewe, Bwana. Tunakungojea. “Wao wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya.” Nasi tunakuomba Wewe utumegee Mkate wa Uzima. Jalia Roho Mtakatifu ayachukue haya Maneno machache, ayapande kwenye kilindi cha moyo. Wape nguvu hao, Bwana, walio wanyonge. Na uwape raha hao walio na nguvu; ujasiri kwa wale walioishiwa na ujasiri; afya kwa wale walio wagonjwa; wokovu kwa wale waliopotea. Nasi tutaviinamisha vichwa vyetu na kukupa Wewe sifa. Tunaomba, na kujikabidhi, pamoja na Neno, katika Jina la Yesu. Amina.

⁵⁰ Ningetaka kukumbukwa na kanisa hili tunapoanza juma lijalo, sasa, katika safari ya kupitia mataifa mawili, kuihubiri Injili. Tuombeeni tunapoenda. Nanyi mkiwa na marafiki wowote huku, mnaijua ratiba, kuja mikutanoni, tungekuwa... ama wangeweza kuja, tutafurahi kuwa nao mkutanoni.

⁵¹ Tutakuwa tukiwaombea ninyi nyote hapa, mchungaji wenu na wengine mbalimbali wanaoidumisha mioto ya nyumbani ikiwaka sasa mpaka tunapoweza kurudi tena. Yesu akiya kabla hatujarudi, tutakutana nanyi kwenye Asubuhi ile. Iwapo tuna kusudi lolote lingine ila hilo, Mungu atusamehe.

⁵² Sasa tunataka kufungua, kwa ajili ya maneno machache tu, usiku wa leo, kutoka kwenye Biblia, yanayopatikana katika Kitabu cha Yoshua 24, kifungu cha 14 na kifungu cha 15. Ninataka kusoma kutoka kwenye Neno Lake. Sikilizeni Neno Lake kwa makini. Yoshua 24:14 na 15.

Basi sasa mcheni BWANA mkamtumikie kwa unyofu wa moyo na kweli: na kuiweka mbali miungu ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya gharika, na huko Misri; mkamtumikie BWANA.

Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya gharika, au kwamba ni miungu ya wale Waamori, ambao ninyi mnakaa katika nchi yao: lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA.

⁵³ Bwana abariki kusomwa kwa Maandiko Yake! Ninayo muhtasari hapa ambao ningetaka kuzungumzia kidogo tu. Na ninataka kuchukua somo usiku wa leo, kuliita, mapambano: *Mapambano Kati Ya Mungu Na Shetani*. Na sasa kulifundisha tu kama somo la shule ya Jumapili, kwa kuwa ninayo Maandiko mengi yamewekwa hapa.

⁵⁴ Katika Edeni, Mungu alijua adui Yake na mashambulizi yote ya adui Yake. Sasa, Mungu ni Mungu asiye na kikomo, na Mungu asiye na kikomo ni Ukamilifu wa ukamilifu. Yeye alijua mambo yote kabla hayajakuwako. Na kwa hiyo, kama Mungu huyu asiye na kikomo angaliweza kuangalia mbele (na aliangalia) na kuona mwisho kutoka mwanzo, na kujua kwamba atakuwa na watoto humu duniani, watoto Wake Mwenyewe waliobarikiwa, hivi hamwamini ya kwamba Yeye angewapa kitu kizuri sana angaliweza kutoa?

⁵⁵ Hivi wewe, usiku wa leo, hungewafanyia watoto wako waliokuwa jamaa wadogo wanyonge wasiojiweza, si unajitahidi sana, na kufanya kazi, na kufanya kila uwezalo, kuwapa yaliyo bora kuliko yote uwezayo, ama unayoweza, kuwaandalia watoto hao? Kwa sababu wewe ni baba, mzazi. Na kama hiyo ndiyo ni—ninii... kile ninachoweza kusema, u—ukweli, na wazo la mzazi wa duniani, nao uzazi ulitoka kwa Mungu, kwa sababu Yeye alikuwa ndiye Mzazi wa kwanza, hivi hufikirii kwamba Mungu, akiona kile Shetani angekuwa, yale Shetani angefanya, Yeye aliwapa watoto Wake, na kuwaandalia, kitu kizuri kuliko vyote kingaliweza kutolewa kwao? Akijua shambulizi la adui lingekuwa nini, Mungu aliwakinga watoto Wake. Mnaona?

⁵⁶ Tuchukue vita, wakati jenerali anapotoka kwenda kukutana na jenerali mwingine, katika vita. Naye jenerali huyu, kama yeye ni raia halisi, wa kweli wa taifa hili ambalo anawakilisha... Naye kweli angekuwa, ili kuwa jenerali. Naye, jambo la kwanza, yeye anachunguza mashambulizi ya adui. Anajua atakalofanya, jinsi atakavyofanya kazi, kwa sababu kwa namna fulani alivuka huko na kufanya upelelezi.

⁵⁷ Tunao wapelelezi kila mahali, mwajua. Kunao wapelelezi wa Marekani Uingereza. Kunao wapelelezi wa Marekani Ufaransa. Kuna Wamare... Na wapelelezi wao wa Ujerumani hapa.

Na kunao... Haijalishi jinsi tulivyo marafiki, tungali tuna wapelelezi. Nasi tunapeleleza namna fulani ya—ya silaha za nyuklia. Halafu tukizipata, tunarudi nazo nchini. Halafu, jambo ni kwamba, wanajiandaa. Vita vikitokea, wanajua jinsi ya kumshambulia adui wao. Na kama tunajua...

⁵⁸ Mungu alijua vita hivi vikuu vilikuwa vinakuja, kati ya mema na mabaya, na Yeye alijua yale adui atakayofanya. Yeye alijua jinsi hasa ya kuwaandaa watu Wake. Kwa hiyo tukiangalia, kitu cha kwanza kabisa ambacho Mungu aliwaandalia watoto Wake kilikuwa... Akiwa hana kikomo, Yeye alijua kilichohitajika kumshinda Shetani, wakati wowote, mahali popote, sehemu yoyote, katika hali zozote. Sasa, asingeweza kusema, “Nitawapa kitu fulani *hapa*, na kisha miaka michache baadaye, huenda nikatafiti kitu bora zaidi cha kuwapa, na kisha baada ya miaka michache baadaye.”

⁵⁹ Kama sisi, katika majeshi, ule uta na mshale wa kale, na nyundo kubwa, nyundo ya miamba, halafu kilichofuata kilikuwa ni... Baada ya uta na mshale, likaja goboli, na baada ya goboli ikaja bunduki ya Springfield, na—na sasa si—silaha za atomiki na kadhalika. Mnaona? Tunaendelea kukua zaidi.

⁶⁰ Lakini, Mungu, hapo mwanzo, aliwapa watoto Wake silaha ya atomiki, kwa sababu Yeye ni Mungu asiye na kikomo. Sasa, akiona kutakuwa na mapambano, na kutakuwa na vita, Mungu aliwazatiti watoto Wake kwa risasi zinazofaa, shambulizi lifaalo, namna nzuri ya kila kitu walichohitaji, ambacho kingewafanikisha kotekote kutoka Edeni hadi Kunyakuliwa. Kilikuwa ni kitu gani? Neno. Neno. Hilo ndilo linalomshinda Shetani, ni Neno. Litamshinda popote, sehemu yoyote. Sasa, kwa nini tupende kuweka kitu kingine mahali pake, wakati tayari tunacho kitu kizuri kuliko vyote kilichopo, Neno?

⁶¹ Na sisi tunaona Yesu akiwa duniani, kuthibitisha tu hili lilikuwa ndicho kifaa kizuri kuliko vyote, wakati Shetani alipoingia katika mapambano ya ana kwa ana na Yesu, Yeye hakuunyosha tu mkono kwa Nguvu Zake na kuifunga mikono yake. Alichukua tu silaha ile ile ambayo Mungu alitoa katika bustani ya Edeni, Neno Lake, na akasema, “Imeandikwa... Imeandikwa...” Naye akampiga konde moja kwa moja akamwondosha kwenye ulingo, kwa Hilo, hiyo ni kweli, kwa kuwa Ndilo la Mungu lililo bora kuliko yote.

⁶² Basi angalieni mahali lilipo. Sio tu la mtu mmoja ama wawili, katika kanisa. Ni kwa ajili ya kila mmoja wetu. Kila mwaminio anayo haki ya kuchukua Neno hili na kupigana na adui popote unapokutana naye. Popote unapokutana na adui, Neno hili ndilo unalopaswa kutumia. Naye Yesu alithibitisha hilo wakati alipokuja. Kwa hiyo aliwaandaa watoto Wake kwa Neno, kwa ajili ya ulinzi wao dhidi ya adui. Wakati vita vikali sana vinapotokea, na mashambulizi, na askari wamejipanga

tayari, basi kuna kitu kimoja tu askari halisi anachoweza kutumia, askari halisi Mkristo, hicho ni BWANA ASEMA HIVI. Atatoka moja kwa moja huko nje na kukabiliana na adui, akiwa na hakikisho kwamba hakuna kitu. . . “Maelfu wanaweza kuanguka mkono wako wa kulia, na elfu kumi mkono wa kushoto, bali hawatakukaribia.” Kumbukeni tu kwamba Mungu alitoa tamshi hili, na kuwapa Hili watoto Wake, na Ndilo zuri kuliko yote yaliyopata kuwapo.

⁶³ Shetani, huko Edeni, wakati alipokuja mara ya kwanza kwenye shambulizi hili, kumshambulia mtu, akijua watoto wa Mungu walilindwa kwa Neno hili, Shetani alilishambulia Neno. Mnaona? Yeye hakumshambulia huyo mtu. Alilishambulia Neno, kwanza.

⁶⁴ Mwangelie huyo mjanja, mjusti, yale afanyayo leo hii. Jambo la kwanza, hawezi kuliweka juu yake, aseme, “Vema, huyo si mtu mzuri.” Huyo ni mtu mzuri. Mnaona? Lakini jambo pekee analojaribu kufanya, haijalishi huyo mtu ni mzuri jinsi gani, ni kuwafanya walikane Neno. Hilo ndilo jambo tu analotaka kufanya, kukufanya ulikane hilo Neno.

⁶⁵ Kwa hiyo Shetani alijaribu ku—kulishambulia Neno, katika bustani ya Edeni. Kwa hiyo ilimbidi kuwa na kitu fulani sasa ambacho angeweza kutumia, kwa—kwa mwanadamu, ambacho kingeonekana bora kuliko Neno hilo. Mnaona? Ilimbidi awe na kitu ambacho kingeonekana bora zaidi, kwa mwanadamu, kuliko Neno. Basi mnajua ni nini alichotumia? *Kutoa hoja*, kile tu tunganese, “maarifa ya kawaida.” Mnaona? Kwa hiyo hiyo ndiyo aliyotumia, naye akafaulu, kwa hiyo hiyo ndiyo ametumia, wakati wote.

⁶⁶ Lakini Mungu hawezi kutoa kitu chochote kingine ila Neno Lake, kwa sababu hilo ndilo alilochagua kwanza. Basi wakati Mungu anapofanya uamuzi, hauna budi kudumu vivyo hivyo.

⁶⁷ Naye Shetani alichukua hoja, na kuchukua hoja na kulishambulia Neno, ndipo akamtikisa Hawa akamwondoa njiani, hiyo ni kweli, kwa kutoa hoja, hoja za kibinadamu.

⁶⁸ Sasa, njia pekee ambayo yeye, mwanamke angaliweza kupata kutokuliamini Neno la Mungu, ilibidi iwe ni ya kuvutia. Naye Shetani anajua jinsi ya kufanya hoja zivutie. Haina budi kukuvutia. Nayo dhambi inavutia sana. Na kunayo dhambi moja tu, na hiyo ni kutokuamini. Kwa hiyo inavutia sana. Shetani huifanya dhambi ivutie sana kwako!

⁶⁹ Nasimama tu hapa kwa dakika chache. Mara nyingi nimewazia, kama kijana, na kusoma juu ya mataifa mbalimbali, na maadili ya nchi. Nami niliwasikia watu mbalimbali wakiniambia sana sana kuhusu huko chini Ufaransa, huko chini mahali panapoitwa Pigalle, na jinsi ambavyo wa—watu walikuwa ni watovu wa uadilifu sana. Vema, nikawazia, “Kama nikiwahi kwenda kule, nitawaona hao watu huko chini,

wanawake wakitoka nje, mwajua, wapotovu, wenye maskini mwonekano wa kichawi kwelikweli, mwajua, na wachoyo.” Basi—basi nikashuka kwenda Pigalle, usiku wa kwanza, mimi na wahudumu wengine watatu. Ndugu, ni mshangao wa jinsi gani tuliopata! Sasa, Shetani ni mwerevu sana kwa jambo hilo. Yeye hatatoa kitu kama hicho. Lakini baadhi ya wasichana warembo kuliko wote niliopata kuona maishani mwangu walikuwa pale, wenye kuvutia. Hakika.

⁷⁰ Dhambi inavutia na inapendeza. Shetani hana kwato zilizogawanyika, na—na—na mkia uliochongoka, na—na namna hiyo. Yeye si maskini John Barleycorn huko nje, mwenye koti linalonging’nia, na—na masikio yanayoning’inia chini. Yeye ni mjanja, anavutia. Dhambi si fidhuli tu, kama mnavyofikiri ilivyo. Inavutia sana. Kwa hiyo, hatuna budi kuiangalia kwa makini. Tatalifikia tu hilo katika muda mfupi. Niliwazia juu ya jambo lingine. Kwa hiyo, jinsi ambavyo Shetani huifanya ione kane halisi sana, inavutia kwao.

⁷¹ Lakini kama wangelikaa tu wamelindwa kwa Neno, waache Neno liwe ngome yao, basi, mnaona, wangelindwa. Wangelikuwa nyuma ya Neno. Neno lingalikuwa mbele yao, sikuzote, BWANA ASEMA HIVI. “BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI.” Kulia ama kushoto, “BWANA ASEMA HIVI.”

⁷² Kama wale Malaika kule chini siku ile, wakati Isaya alipowakuta hekaluni. Alidhani alikuwa akipiga hatua vizuri sana; mhubiri mzuri kiasi. Mfalme alimpenda vizuri sana, lakini huyo mfalme aliondolewa kwake siku moja. Ndipo akapiga magoti madhabahuni na kuingia katika ono, akawaona Malaika wakiwa na mabawa juu ya nyuso Zao, na juu ya miguu Yao, huku wanaruka kwa mabawa mawili, wakiimba, “Mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi,” mnaona, kila njia waliyoendea.

⁷³ Ezekieli aliona picha ya hilo ono. Roho wa Mungu alipokuwa akienda *huku*, alikuwa na uso wa maksai. *Huku*, Yeye alikuwa na uso wa simba. Na popote alipoenda, alikuwa na uso. Popote alipoenda, alikuwa amelindwa.

⁷⁴ Neno la Mungu, hakuna njia ya kulizunguka. Limelindwa, kote kote, kila mahali, “BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI.” Matembezi yako, mazungumzo yako, biashara yako, shirika lako, na kila kitu, liweke Neno la Mungu kwanza.

⁷⁵ Unasema, “Ninaamini nitaenda usiku wa leo, na dansi hili dogo tu halitamdhuru mtu yeyote.” Ungeweza kuchukua BWANA ASEMA HIVI pamoja nawe? Unaona? Unaona? “Ninaamini kama ningeamilisha biashara hii, loo, kidogo ina hila.” Lakini ungeweza kusema “BWANA ASEMA HIVI” pamoja nayo? Unaona?

⁷⁶ Daima mchukue Yeye kwanza, dumu ngomeni, kwa kuwa Yeye ndiye ngome yetu, mkazo wake.

⁷⁷ Lakini unajua inakubidi kupuuza, kabla...Ili kuuamini uongo wa ibilisi, inakubidi kupuuza na kuikana Kweli ya Mungu, kwanza, kabla ya kuweza kuamini uongo wa ibilisi. Ulipata kuwazia hilo? Inakubidi kuukana Ukweli, kwanza, kabla hujaweza kuamini uongo. Kweli. Inakubidi kuukana Huo!

⁷⁸ Hawa aliondoka nyuma Yake, akashindwa vita. Mara Hawa...Shetani alikuwa amesimama huko nje, akipiga shabaha zake. Akasema, "Lakini Bwana alisema..." Ndipo akapiga tena. Akasema, "Lakini Bwana alisema..." Kwa hiyo basi akapiga tena, kwa njia nyingine. "Lakini Bwana alisema..."

⁷⁹ Lakini Shetani akainuka huko nyuma, kasema, "Lakini ngoja kidogo. Kama Bwana kweli alisema Hilo, hebu nikwambie jambo fulani. Unaona, wewe si mwenye hekima kama Mungu. Hujui mema na mabaya. Lakini kama...Sikiza. Hivi hungetaka kuwa na hekima kama Mungu?"

⁸⁰ "Mbona," Hawa akasema, "naam, na—na—na—naamini ningependa." Labda kitu kama hicho. "Ninaamini ningetaka kujua tu hekima yote ya Mungu. Ningetaka kujua mema na mabaya. Siyajui."

"Vema, nitakwambia."

Sasa, yeye akasema, "Lakini, lakini, Bwana alisema..."

⁸¹ "Vema, lakini, hakika, unajua Yeye ni Mungu mwema. Yeye hatafanya hivyo." Unaona?

⁸² Papo hapo akalitoboa tundu, apate kurushia risasi. Papo hapo akachukua hatua mbaya, papo hapo, akasimama kidogo.

⁸³ Sasa hebu niseme jambo fulani kuhusu ninyi Wakristo hapa chini. Kamwe usisimame sekunde moja kwa ajili ya ibilisi. Usisimame kutoa hoja Kwake. Unapoanza kuitolea hoja, ibilisi anaingia ndani moja kwa moja. Huwezi kumtolea Mungu hoja. Huwezi kumwelewa Mungu. Inakubidi tu kumwamini Mungu. Mnaona? Siwezi kumwelezea Mungu. Hakuna mtu anayeweza. Siwezi kuyaelezea mambo mengi. Lakini, jambo pekee, ninaliamini tu Hilo, kwa sababu Yeye alisema hivyo. Sasa, hakuna mmoja wetu anayeweza kulielezea Hilo. Usijaribu kulielezea Hilo.

⁸⁴ Usiambatane na hawa wasioamini wasemao, "Vema, sasa angalieni, mchungaji wenu huko nje, Junior, ninamsikia akiwaombea wagonjwa. Sasa ninyi nyote mna kichaa huko chini. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu."

⁸⁵ Sema, "Vema, haupo kwa ajili yako, basi. Wewe ni asiyeamini." Kisha usonge mbele tu moja kwa moja. Mnaona? Ni kwa ajili ya waaminio pekee. Mnaona? Msininii...

⁸⁶ "Vema, nyote mnasema mna Roho Mtakatifu. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu."

Aisee, “Si kwa ajili yako wewe, basi. Ni kwa ajili yangu.” Endelea tu. Unaona? Unaona?

⁸⁷ Usitoe hoja. Usijaribu kulitolea hoja. Halina hoja zozote. Liamini tu. Usitoe hoja hata kidogo. Kwa sababu, kumbuka, njia pekee unayoweza kumkubali Mungu ni kwa imani, sio kwa kutoa hoja, sio kwa ufahamu, sio kwa kuweza kuelezea. Huelezei chochote. Unaamini kitu Fulani. Sio vile unavyojisikia. Yesu kamwe hakusema, “Ulilihisi Hilo?” Alisema, “Uliliamini Hilo?” Hiyo ni kweli. Unaamini tu yale Mungu aliyosema. Siwezi kuwaelezea jinsi wao... Jinsi ambavyo ninii... Mwujiza ulio mkuu kuliko yote ninaoweza kuwazia, ni mtu ambaye...

⁸⁸ Kama tu vile, umchukue nguruwe, na umwambie nguruwe huyo, “Unajua, wewe si nguruwe tena. Wewe ni mwana-kondoo,” naye anakuwa mwana-kondoo. Mnaona? Hilo lingekuwa ni gumu kuamini.

⁸⁹ Vema, ni jambo lile lile linalotendeka unapoongoka kutoka mwenye dhambi ukawa Mkristo. Unaona? Linabadilisha maoni yako mwenyewe. Linabadilisha mapenzi yako mwenyewe. Linabadilisha kila kitu kilicho ndani yako. Nalo linakuingiza katika maisha mengine, na kukupa Roho nyingine, inayotoa ushuhuda mwingine. Unaona? Ndipo maisha yako ya kale hayana budi kufa, na mapya hayana budi kuzaliwa mara ya pili. Halafu basi, unaona, wewe si kiumbe ulichokuwa tena, hata kidogo. Hapo ndipo unapokuja nyuma ya ile Damu, umelindwa ngomeni kwa Neno. Usijaribu kuelezea chochote, liamini tu na uendele. “Bwana, naamini. Mwokozi, inua imani yangu Kwako, hata iweze kuhamisha mlima.” Mnaona? “Bwana, ninaamini, kwa kuwa mashaka yangu yote yamezikwa kwenye ile Chemchemi.”

⁹⁰ Vipi kama Ibrahimu alikuwa ameulizwa, madaktari walikuwa wamekuja, kasema, “Ibrahimu, wewe una umri wa miaka mia moja. Mke wako ana tisini. Utapataje mtoto?”

⁹¹ Sasa, Ibrahimu aseme, “Vema, sasa, nitakwambia, mambo yako *hivi*. Unaona, unakuja wakati ambapo tutakunywa kitu fulani, na hiki kitafanya *hivi*. Na badiliko la namna hii linaenda...” Ibrahimu asingeweza kuelezea hilo.

⁹² Ibrahimu angalisema kitu kama, “Sijui. Sijui zaidi kulihusu kuliko unavyojua wewe. Jambo pekee ninalotulia juu yake, ni, Yeye alisema tutampata. Nami ninamtazamia.” Jambo ndilo hilo. Naam, bwana.

⁹³ Sasa, hilo ndilo tu linalohitajika. Lichukue tu, liamini. “Mungu alisema hivyo.” Na hilo—hilo linatatua jambo hilo lote, kwa sababu Mungu alilisema Hilo.

⁹⁴ Sasa, tunaona, Hawa kushindwa vitani, aliondoka nyuma ya hilo Neno, akasimama juu ya handaki na kusema, “Ati wasemaje? Hiyo ni Kweli?” Amepotea, papo hapo.

95 “Vema, wajua, hatufundishi Hilo kanisani mwetu. Tunaamini yale aliyosema Yeye *hapa*.”

96 “Naam, lakini, sikiliza, kipenzi, unajua vema zaidi ya Hilo. Maarifa yako mwenyewe ya kawaida yangekwambia ya kwamba Hilo si kweli. Mbona, niliwasikia hao watu wakilia tu na kulia. Wanalilia nini? Unaona? Sasa, maarifa yako mwenyewe ya kawaida yangukuonyesha ya kwamba wamesisimkwa tu. Wana mhemko. Mnaona?” Kama ukisimama kusikiliza hayo, umepoteza vita.

97 Kama wakisema, “Loo, sasa, ngoja kidogo. Daktari wako alisema hivyo, kwamba ulikuwa na TB. Nayo i—imeenea sana. Hakuna njia kamwe ya wewe kuimudu hiyo TB. Daktari alisema hakuna. Sasa, si maarifa ya kawaida yanasema hivyo?” Vema, kama utategemea kutoa hoja, afadhali uwe tayari kufa.

98 Lakini kama unaendea yale Bwana aliyotoa, ile ahadi, nawe unaweza kuamini Hiyo, inabadilisha mpango wote.

99 Sasa, jinsi inavyobadilisha, ndivyo ilivyonibadilishia mimi huko chini. Mnaona? Ninaliamini tu. Sijui ilivyotendeka, lakini palikuwapo na kiumbe kipya kilichokuja. Nilizoea, ningelikwepa kanisa. Ni- . . .

100 Jamaa fulani aliniambia, wakati nilipokuwa nikipigana ngumi, tulikuwa . . . Nilikuwa nikipigania mashindano yangu ya kumi na tano ya weledi, huku chini katika—katika Evansville, Indiana. Naye Howard McClain, wengi wenu watu wa New Albany mlimfahamu kule. Basi tulikuwa tukitembea mtaani. Naye Howard alikuwa wa uzito wa wastani, nami nilikuwa wa uzito wa bantamu. Nilikuwa nikipigana na Billy Frick kutoka Huntington, Virginia ya Magharibi. Nilikuwa nimevaa suti ya samawati, kama hii. Katika siku hizo, nilikuwa na nywele kidogo. Basi nilikuwa nikitembea mtaani. Tungekula chakula cha jioni yapata saa tisa, tujiandae kwa mapigano usiku huo. Tulikuwa tukiingia basi tukapumzike, na kisha mikono yetu ifungwe. Ndipo Howard akaniambia, kasema, “Unajua nini, Bill?”

Nikasema, “Ati nini?”

Kasema, “Unaonekana kama maskini mhubiri wa Kibaptisti.”

101 Naye angaliweza kuniita chochote. Kamwe mimi . . . Nikageuka, nikasema, “Sasa, ngoja kidogo, Howard. Sasa, wewe ulicheka uliposema hivyo.” Mimi, nikiwa na urefu *huu*, bali nilikuwa tayari kupanda juu yake. Sikutaka uhusiano wowote na mhubiri.

102 Na sasa sifa kubwa kuliko zote angaliweza kunipa mimi, loo, mtu fulani aliposema, “Ndugu Branham, unaonekana kama mhubiri.”

Nasema, “Mungu asifiwe!” Unaona? Unaona?

¹⁰³ Kuna shida gani? Nilikufa. Nami ni kiumbe kipya. Nilifanyaje jambo hilo? Nililichukua Neno Lake. “Ndugu Branham, ni dawa ya aina gani, ni fomula gani uliyokunywa?” Sikunywa yoyote. “Yeye alifanyaje hilo?” Sijui. Lakini, kwa vyovyote vile, nililiamini. Sikunywa chochote. Nililiamini tu. Basi Yeye aliniinua kutoka kile nilichokuwa, mwenye dhambi, nikawa Mkristo. Yeye alifanya hilo kwa sababu nililichukua Neno Lake. Atafanya jambo lilo hilo kwa maradhi. Atafanya jambo lilo hilo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Atafanya jambo lilo hilo kwa ahadi yoyote atakayotoa.

¹⁰⁴ Lakini, mnaona, ni lipi, somo langu ni lipi? Mapambano. Mapambano. Shetani hujaribu kukufanya utoe hoja kulihusu, na wewe kamwe usifanye hivyo.

¹⁰⁵ Lakini ukiisha kuwa Mkristo, basi unalindwa ngomeni kwa Neno na ahadi yoyote katika Neno. Whiu! Sikujua nitasema hilo. Mnaona? Wewe ni, wakati unapokuwa Mkristo, unawekwa nyuma ya Neno la Mungu. Mnaona? Sasa, hiyo hapo ngome yako, usalama. Loo, jamani! Kila ahadi katika Hiyo ni yako. Jambo pekee linalokupasa kufanya ni kunyosha tu mkono na kuipokea, nawe uendelee moja kwa moja nayo. “Unajuaje itafanya kazi?” Sijui jinsi itakavyofanya kazi. “Nielezee.” Sijui. Jambo pekee nijualo, ni kwamba, Mungu aliwapa watoto Wake shambulizi lililo bora kuliko yote wangaliweza kuwa nayo, na kitu kizuri kuliko vyote cha kushambulia nacho, maana Yeye anajua mbinu za adui.

¹⁰⁶ Sasa, hebu—hebu tulibaini hilo vilivyo; kama vile kuchukua kemia ya damu, ama kemia ya maji, ama chochote kile. Mnaona? Hebu—hebu tuichunguze yote. Kwa nini, kwa nini Yeye alilitoa Neno? Kwa sababu. . . Mko tayari? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Neno ni la Milele. Mnaona? Na kama Mungu alifanya ahadi ambayo ni ya Milele, wala hakuna kitu mahali popote kinachoweza kuikomesha. Wasingeweza. Kuipindua kila atomu juu chini, na kuigeuza kinyumenyume, kusingeweza kulitoboa Neno la Mungu, Neno moja dogo. Mnaona? Maana, Yesu alisema, “Mbingu na nchi pia zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” Mnaona? Hilo ndilo silaha nzuri kuliko zote iliyopo. Ni Neno la Mungu wa Milele.

¹⁰⁷ Sasa, Neno la Mungu ni nini? Neno la Mungu ni Mungu Mwenyewe. Kwa hiyo, Mungu alimpa mwaminio Yeye Mwenyewe. Amina. Whiu! Ni Mungu Mwenyewe. Alimpa mwaminio Yeye Mwenyewe, kumshambulia adui kwake. Kwa maneno mengine, Yeye ni Baba. Nalo Neno ni Mungu, basi Neno ni Baba yetu. Tumezaliwa kwa Neno, na Yeye amesimama mstari wa mbele kwa ajili ya watoto Wake. Amina. Haya basi. Yeye amesimama huko nje kwa ajili ya watoto Wake. Tunaogopa nini? Unyakuo ni wa hakika. Kule Kuja ni kwa hakika. Kila baraka iliyoahidiwa ni yetu. Yote ni mali yetu. Sasa, kama kwa namna fulani tukizembea na kusema. . .

¹⁰⁸ Shetani aseme, “Njoo huku, upande *huu*, nitalihoji Hilo pamoja nawe.” Aa-loo, umeenda nyuma ya Baba basi. Unaona? Kamwe usifanye hivyo. Wewe kaa moja kwa moja ambapo Baba amesimama, moja kwa moja mahali linaposema. Linasema, “Ni Baba asema hivi.” Unaona? “Baba yangu asema hivi. Baba yangu asema hivi.” Litamshinda. Hakika kabisa, halina budi kumshinda. Vema.

¹⁰⁹ Lakini unapoondoka nyuma ya Hilo, kama Hawa alivyofanya, umeshindwa vita. Sasa, maskini Hawa, yeye alisikiliza. Akapoteza mahali pake. Vema.

¹¹⁰ Ndipo basi Mungu akawachagua wanaume kuishikilia ngome Yake, na Yeye amefanya hivyo tangu wakati huo.

¹¹¹ Hapo ndipo, mara nyingi, watu katika siku hizi za mwisho wakati mwingine husema, “Kwa nini usingeweza kuwazia kwamba mama huyo angeweza kufanya kazi nzuri tu mimbarani kama mwanamume?” Sibishani na hilo, hata kidogo. Wakati mwingine bora zaidi kuliko vile ningaliweza, wengi wao.

¹¹² Lakini, unaona, hatuna budi kuchukua yale Mungu aliyofanya. Mnaona? Pale pale, Hawa ndiye aliyevunja vizingiti, wala Adamu hakuvunja vizingiti. La, bwana. Lakini kwa sababu alimpenda mke wake, aliondoka moja kwa moja pamoja naye. Mnaona? Kwa hiyo, Mungu aliwachagua wanaume kuishikilia ngome.

¹¹³ Sasa, la pili, tunaona basi, baada ya kuvipoteza vita pale, ule wakati wa maangamizi uliwajia, wakati huo mwingine, kulikuwako na ba—badiliko la vipindi vya wakati, tangu wakati huo.

¹¹⁴ Tunajua jinsi hivyo vita vilivyoenda. Tunajua ya kwamba Hawa alipoteza vita kwa sababu alitegemea hoja zake badala ya imani yake katika Neno la Mungu. Hebu turudie hilo. Yeye alitegemea hoja zake mwenyewe badala ya kuwa na imani katika Neno la Mungu. Alilitolea hoja. Kwa hiyo akaivunja mistari ya mbele naye adui akaingia ndani mbio, ndipo basi mauti yakaupiga ulimwengu. Sasa, kwa hiyo, Mungu kamwe hakuwa na imani nalo tena kwa wanawake, kuushikilia mistari huo wa mbele. Uko na wanaume.

¹¹⁵ Na sasa, kwenye badiliko hilo lingine la kipindi cha wakati, mapambano yakaanza. Nami ninayaangalia Maandiko hapa. Ninaamini ya kwamba nitaanza tu na kulisoma.

¹¹⁶ Tuna muda gani kweli, mnahubiri hasa juu ya, wowote tu, yapata tu...Haitachukua yapata tu saa sita zaidi, nasi tutaninii...Na kwa hiyo sisi...Sikumaanisha hilo, jamani. Mimi...

¹¹⁷ Hebu tuanzie hapa, ninyi katika Biblia zenu. Hebu tusome tu dakika chache. Ninapenda tu kulisoma Hili, tunapoendelea, halafu ni Neno la Mungu kote kote. Hebu tuanzie kwenye

badiliko la vipindi vya wakati tena, kutoka kwa Adamu, kipindi cha wakati cha Adamu hata kipindi cha wakati cha Nuhu. Sasa—sasa kabla tu wakati huo haujafika, hebu tuangalie tu yale—yale yaliyotukia. Hebu tuanzie, tuanzie kwenye mlango wa 6 wa Mwanzo, na tusome tu vifungu vichache.

Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao,

Na wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wowote waliowachagua.

118 Sasa hebu tulinganishe tu hilo. Sasa, kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sasa angalieni, tukisoma hili kwa makini sasa, kama tu somo la shule ya Jumapili, kwa kifungu kimoja tu ama viwili, kisha nitaendelea moja kwa moja pamoja na Maandiko mengine zaidi.

...ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni... nchi na wana wa kike wakazaliwa kwao wanadamu, mnaona,

...wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu...

119 Sasa, mliliona hilo?

...wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wowote waliowachagua...wowote waliowachagua.

120 Sasa, wengi sana wa wanatheolojia...Sitaki kuwa tofauti. Simaanishi kuwa. Lakini wengi wenu mnajua kwamba wanatheolojia wanaamini, kwamba, “Hawa malaika walioanguka, waliokuwa wameanguka kwa uongo wa Lusifa, walijitwalia wake. Walikuwa malaika walioanguka, kwa kweli wana wa Mungu, walioanguka kutoka kwa neema, wakatupwa duniani, wakajingiza katika mwili, kisha wakajitwalia wake.” Kidogo si—sidhani hilo huambatanisha hoja na Maandiko.

121 Kwa sababu, kwanza, kabla malaika aliyeanguka hajaweza kujifanya mwanadamu, ingembidi kwanza kuwa ni muumbaji. Na kuna Muumba mmoja tu, na huyo ni Mungu. Kwa hiyo hilo lingelifagilia mbali.

122 Jambo jingine, “Wana wa Mungu walijitwalia binti za wanadamu.” Basi mljua, Biblia kamwe haionyeshi jinsia za malaika? Mnaona? Hakuna kuonyesha jinsia katika malaika. Wala hakuna mahali katika Biblia palipo na malaika mwanamke. Kwa sababu, mwanamke ni zaotuka la mwanamume. Wote wangekuwa ni sawa, kama vile Adamu alivyokuwa wote wawili Adamu na Hawa, kwa kuanzia. Mnaona? Yeye alitolewa ubavuni mwake. Kwa hiyo i—

inatupilia mbali hoja yao, kwamba hawa walikuwa ni malaika walioanguka.

¹²³ Lakini ikiwa mtaniruhusu, na msijaribu kuwazia kwamba ninajaribu kujifanya mjua yote hapa, lakini kutoa tu wa—wazo langu kulihusu. Nafikiri, “Hawa wana wa Mungu walikuwa ni wana wa Sethi, waliowaona binti za Wakaini, wa Kaini, kwamba walikuwa wazuri.” Kwa sababu, “Wana wa Sethi walikuja, walikuwa ni wana wa Adamu, ambaye alikuwa ni mwana wa Mungu.” Lakini, “Mwana, binti za Kaini, ambaye alikuwa ni mwana wa Shetani.”

¹²⁴ Sasa, mnaona, “Waliona,” mwishoni tu, kabla ya maangamizi haya yaliyoitangulia gharika, “kwamba binti za Wakaini walikuwa wazuri, warembo, wanaovutia.” Mnalipata?

¹²⁵ Sasa, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu,” wanawake, warembo. Wanawake wa namna gani? Wakaini, mnaona, wakiwachukua wana wa Mungu. Mnaona? “Wana wa Mungu wakiwachukua wanawake Wakaini.”

¹²⁶ Urembo wa kupindukia wa wanawake umeongezeka sana katika miaka hamsini iliyopita; kuchukua picha ya miaka hamsini iliyopita, jinsi mwanamke m—mrembo alivyoonekana. Nilikuwa nikiangalia, hivi majuzi, katika historia ya vita; na jinsi ambavyo Pearl White, yapata miaka mia moja iliyopita, wakati alipodungwa kisu na Scott Jackson, mpenzi wake, na sura ya huyo mwanamke. Sasa, pia, ya Mary Bonneville, na wengi wa wanaojiiita wanawake warembo, wa miaka hamsini hadi mia moja iliyopita, ukiwalinganisha na wanawake siku hizi. Wasingeweza kusimama kwenye kivuli. La, hasha. Maungo makakamavu!

¹²⁷ Wanawake wamekuwa vidosho, uanawake, na kadhalika, wanavutia zaidi. Basi ni kitu gani? Wanajivalisha wapate kutamanisha zaidi. Ambapo, wanawake walikuwa wakivaa nguo kubwa, na za mikono, na sketi ndefu, na kuficha mwili wao kwa maana hawakutaka wanaume wawatamani. Walimwishia mwanamume mmoja aliyewachagua kama mke. Siku hizi, wanawake wanajimwaga katika nguo ndogo sana, na upotovu wa maadili unaendelea sana na kufanya ghasia hata li—limepita kuwazia.

¹²⁸ Lilikuwa la kustaajabisha sana, niliposoma uchambuzi hivi majuzi, wa Chicago, nilipokuwa kule. New York, Los Angeles, Birmingham, na—na mingi ya miji mikuu sana, kwenye kilabu hiki, juu ya vilabu vya anasa, wamekusanyika hivi kwamba familia baada ya familia, kote katika ujirani, wanajiunga na kilabu hiki. Nao wanaingia mahali fulani pa mkutano, wanachukua funguo zao, wanazitupa ndani ya kofia, mwanamke ananyosha mkono na kuchukua ufunguo na huyo ndiye mume

wake mpaka watakapokutana tena. Hao ni wanawake wetu wa Marekani.

¹²⁹ Unaona, inaonyesha ya kwamba, imerudi tena, ilianza hapo mwanzo na wanawake, kwa kujuana kimwili, nayo inaishia vivyo hivyo mwishoni sasa. Sio. . .

¹³⁰ Mungu hakuibariki, kwa ajili ya mwanamke mwaminifu na mwema. Soma katika Isaya, wakati aliposema jinsi ambavyo wale watakaoepuka katika siku za mwisho, binti za Sayuni watakaojepusha na mambo haya mabaya sana yaliyo juu ya nchi.

¹³¹ Sasa, “Wana wa Mungu waliwaona binti za wanadamu ya kuwa walikuwa ni wazuri; nao wakajitwalia wake, wote waliowachagua,” sasa ishara kuu ya wakati wa mwisho. Hebu tusome kifungu kingine.

BWANA akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, . . .

¹³² Mara baada ya haya kutukia, kuoana. Luka anatwambia hayo. Ninalo limeandikwa hapa. Nafikiri Luka 7:27 ilisema kwamba, jinsi. . . Ama, Luka 17:27 ilisema kwamba, jinsi ambavyo, “Walioa na kuolewa, katika siku za Nuhu.” Mnaona jinsi ilivyokuwa? Jambo lile lile. Wanaume waliangalia kule kuvutia. “Wana wa Mungu,” waliodhaniwa wanaishikilia ngome, “waliwaangalia binti za wanadamu—wanadamu,” jinsi walivyokuwa wa kuvutia sana, wazuri. “Nao wakajitwalia wanawake, nao wakawaoa, na wakaolewa.” Jambo lile lile wanalofanya siku hizi. Mnaona?

BWANA akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama: basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini.

Na wanafeli walikuwa duniani siku zile; tena baada ya hayo, wana wa Mungu walipoingia . . . kwenye binti za wanadamu, wakazaa nao watoto, nao hao ndio watu waliokuwa hodari zamani, watu . . . wenye sifa.

¹³³ Angalieni. Wanawake hawa Wakaini werevu, wenye elimu, sio. . . kutoka kwenye ukoo wa Kaini, waliolewa na hawa wavulana wakulima wadogo wanyenyekevu wa Sethi. Na kutoka hapo, wakawa “majitu” na wakawa wenye “sifa.” Tunaona ya kwamba walikuwa wanasayansi mashuhuri, mafundi hodari wa mbao. Watu mashuhuri, werevu, wenye elimu, nao walikuwa na u—uchumi mkuu. Nao waliishi katika wakati mkuu sana wa kisayansi hata wakazijenga piramidi ambazo tusingeweza kujenga siku hizi. Walijenga sfiniksi na vivutio vingi vikubwa tunavyoviona kwenye miamba, zamani za kale, ambavyo tusingeweza kujenga siku hizi. Kwa sababu, watu hao walitegemea maarifa yao, nao wakawa wanasayansi na watu werevu, na watu wenye sifa.

134 Lakini wana wa Mungu, waliodumu wanyenyekevu, walikaa mbali na mambo kama hayo, wakamtegemea Mungu, wakijua ya kwamba watarithi vitu vyote hatimaye. Mnaona?

135 Kwa hiyo watu siku hizi wanasema, “Wao ni werevu. Wana *haya* yote. Tunafanya *haya yote*.” Werevu sana kuliko tulivyokuwa sisi, nasi tuko mbali sana na Mungu kuliko tulivyokuwa. Mnaona? Unajiondoa mwenyewe moja kwa moja. Vema.

136 Sitachukua wakati mwingine kuendelea kusoma. Wakati mwingine, mkipata nafasi, endeleeni kusoma, mlango wa 6 wa Mwanzo, jinsi ambavyo mambo hayo yalitukia.

137 Alama ndogo tu, nilifikiri nitasoma hilo. Nilikuwa nimeandika hapa, kwamba nitasoma hilo, kifungu kimoja tu ama viwili, kuwaonyesha usambamba wa wakati wa Nuhu na wakati huu. Sasa, tunaona kwamba watu wanaoa na kuolewa. Tunaona urembo wa wanawake, ambao wamevua nguo zao, wapate kuwa wa kuvutia kwa wana wa Mungu.

138 Sasa, sio tu kuiweka sehemu hii ya Ujumbe juu ya wanawake. Ninashukuru kuwa na wanawake kama walio hapa, ambao ni kina mama wa heshima, wasichana ambao wangali ni waadilifu na wa heshima. Ambao hawavai. . .

139 Sasa, mwa—mwanamke wa kawaida, siku hizi, amerudi kwenye majani ya mitini, kama tu Hawa alivyokuwa. Nalo “jani la mtini” kweli ni mfumo uliobuniwa na mwanadamu; kaptura, kuvuta sigara, nywele zilizokatwa, kuvutia. Wangefanya hivyo kwa sababu gani, ati wapate kuonekana kwa mume wao? Kama wakifanya hivyo, basi yeye si mwana wa Mungu; yeye ni Mkaini. Halafu kama yeye ni mwana wa Mungu, yeye atakwambia, “Usafishe uso wako na uvae nguo.” Unaona? Kweli.

140 Sasa, Mungu, katika wakati huu, Yeye alichagua kulituma Neno Lake tena, kwa ajili ya watoto Wake. Ndipo akamchagua nabii. “Nalo Neno la Bwana huwajia manabii.” Naye Nuhu na Henoko, ni mfano mzuri jinsi gani! Naye mtu fulani. . . Mara nyingi, watu. . .

141 Na—naona, baadhi ya hayo maswali sikuyajibu. Waliuliza swali hilo. Kasema, “Ndugu Branham, sikubaliani nawe.” Huyu ndugu wa thamani ambaye aliandika baadhi ya makala mazuri sana, ambayo ninaendea sasa. Ndugu. . . Jina la jamaa huyo ni nani, tunaenda kumhubiria, huko juu sasa, mkutano huu unaofuata huku juu kwenye Pine ya Kusini, ama Pine ya Kusini? [Mtu fulani anasema, “Parker.”—Mh.] Parker. Thomas Parker, yeye alisema, “Lipo jambo ambalo sina budi kutokukubaliana na Ndugu Branham.” Kasema, “Yeye anaamini ya kwamba Kanisa halitapitia kwenye ile Dhiki.” Kasema, “Ninaamini Kanisa linapitia kwenye ile Dhiki, kwa ajili ya utakaso.” Ilikuwa je na Damu ya Yesu basi? Mnaona? Hakuna mahali

katika mfano wowote, ama katika Neno lolote, ambapo Kanisa linapitia kwenye ile Dhiki.

¹⁴² [Mtu fulani anaondoa upepeo—Mh.] Inawabidi kuuweka huo juu ya watu hawa wasio na upara, hawapwelewi na sauti upesi sana.

¹⁴³ Hakuna mahali ambapo Kanisa linapitia kwenye kipindi cha ile Dhiki kamwe. Damu ya Kristo, na utimilifu wa matumizi ya Damu ya Yesu Kristo, husafisha dhambi yote. Basi kwa nini itubidi kutakaswa? Tunatakaswa kila siku; hakuna Dhiki. Sikilizeni. Sikilizeni yale Yesu aliyosema katika Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Amina.

¹⁴⁴ Henoko, nabii! Nuhu ni mfano wa Wayahudi, masalio, mtumishi wa Mungu. Naye Henoko, yule nabii mkuu aliyetabiri juu ya kuja kwa Bwana, aliamishwa, akanyakuliwa kabla ya ile gharika. Nuhu alipitishwa mle, apate kuhifadhi uzao duniani.

¹⁴⁵ Sasa, Mungu alilituma Neno Lake kwa nabii Wake, Nuhu, na wakati Nuhu na Henoko walipoanza kutabiri. Halafu basi kabla tu ya ile gharika kupiga, kulifanyika nini? Henoko alipaa juu; Nuhu akapitia mle. Mnaona? Henoko aliamishwa. Ishara ya Nuhu, ilikuwa, kumtazama Henoko. Wakati Henoko alipokosekana, basi Nuhu akajua gharika ilikuwa imekaribia, maana alikuwa akimtazama Henoko.

¹⁴⁶ Sasa, Shetani, katika wakati huu, aliweka mfumo ule ule aliouweka katika bustani ya Edeni, akitoa hoja dhidi ya Neno la manabii hawa. Jambo lile lile! Sasa, Shetani aliweka mfumo wake. Alikuwa na zaidi ya mtu mmoja ama wawili wa kuwashughulikia sasa; alikuwa na mabilioni wa kuwashughulikia. Wakati uliotangulia ile gharika, watu wengi zaidi, labda, kuliko walivyo sasa. Waliongezeka, kote kwenye uso wa dunia. Kulikuwako na halaiki kubwa ya watu nyakati hizo, labla wengi zaidi kuliko walioko sasa. Basi sasa angalieni. Shetani, kusudi, (sio udanganyifu wa mmoja, kwa Hawa), yeye alijiundia mfumo. Ulikuwa ni kitu gani? Kulishambulia Neno la Bwana lililowajia manabii. Mnalipata? Yeye hutumia mbinu iyo hiyo ya kale, kila wakati. Naye Mungu hudumu na Lake lile lile, Neno.

¹⁴⁷ Hawa hapa Nuhu na Henoko wanakuja, wakiwa na BWANA ASEMA HIVI, wakijenga safina. Sasa, angalieni, mfumo wa Shetani uliucheka mfumo wa Mungu. Sasa linganisha hilo na leo hii, “watakatifu wanaojibingirisha,” na kadhalika. Mnaona? Wenye kudhihaki, Biblia ilisema, waliucheka mfumo wa Mungu. Mfumo wa Shetani uliucheka mfumo wa Mungu. Walidhani haukustahimili sayansi yao wenyewe na hoja zao.

148 Sasa, wao walisema, “Maskini jamaa huyo huko juu kilimani, akiijenga ile safina, naye anasema kuna maji yanayoshuka chini kutoka *huko* juu. Sasa, tuna wanasayansi walio bora zaidi ulimwenguni. Sasa, labda wanayo rada ambayo wanaweza kuirusha moja kwa moja hata mwezini, na kadhalika, nao wanaweza kuthibitisha kwamba hamna maji mle. Sasa, kunakuwaje na yoyote yakishuka chini? Ewe mzee, una kichaa.”

“Lakini nina BWANA ASEMA HIVI.” Akaijenga moja kwa moja.

149 Akasimama moja kwa moja mlangoni mwa safina, akiihubiri Injili, na kujenga, na kumwangalia Henoko. Wakati alipoingia, jioni moja, alisema, “Waliuchukua, huko chini?”

150 “La. Walinicheka. Walinitupia mayai yaliyooza, na mambo yote mengine.”

151 “Walifanya jambo lile lile hapa juu. Lakini hebu tuijenge kwa bidii moja kwa moja.” Mnaona? “Loo, wananiita ‘mtakatifu anayejibingirisha,’ na mambo yote mengine, bali hilo ni sawa.”

152 Wote walikusanyika ndani kwa ajili ya mkutano wa maombi, nao wakaendelea vivyo hivyo, mnaona, vile hasa inavyofanya siku hizi. Kwa sababu, walijua walikuwa wamelindwa, kwa sababu walikuwa wamesimama nyuma ya BWANA ASEMA HIVI.

153 Sasa, mtoa hoja wa kawaida angesema, “Loo, huo ni upuuzi.” Mwanamke fulani wakati mmoja alisema . . .

154 Wakati mmoja nilikuwa . . . Mvulana huyu alifundisha shule ya Jumapili kwenye kanisa la Kibaptisti. Nilikuwa nikihubiri huko juu, usiku mmoja. Nami nikakutana naye katikati ya mji; nilikuwa nikiendesha baiskeli yangu. Mimi, katikati ya mji, nilikutana naye. Alikuwa akiendesha baiskeli. Akasimama kando. Akasema, “Billy, nilikuja kukusikiliza hivi majuzi usiku.” Kisha kasema, “Nilikuwa nikifurahia yale uliyokuwa ukisema mpaka mwanamke yule alipoanza kulia na kupiga makelele, hao watu wote wakisema, ‘Amina.’” Kisha kasema, “Kamwe nisingeweza kuvumilia hilo.” Mnaona? Akasema, “Lilinipa mtetemo mgongoni mwangu, kuwasikia hao watu, ‘Amina,’ papo hapo ulipokuwa ukisema jambo fulani.”

155 Nikasema, “Ndugu, halikuniathiri hivyo.” Nikasema, “Akasema . . .” Nikasema, “Nitakwambia.” Nikasema, “Kwani huamini katika kusema ‘amina,’ na huko kupaza sauti kidogo na mambo waliyokuwa wakifanya?”

Kasema, “La. Siamini hilo.”

156 Nikasema, “Kama ingetokea ukafika Mbinguni, ungeganda.” Nikasema, “Kwa sababu, hao ni . . . Kama hilo lilisababisha mtetemo kuenea mgongoni mwako, itakuwaje wakati Malaika, huku wamesimama mbele za Mungu, mchana na usiku, wakilia kwa sauti, ‘Mtakatifu, mtakatifu,

mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu?” Mbona, huu ndio ulimwengu mnyamavu kuliko wote utakaowahi kuishi ndani yake. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁷ Katika kuzimu kutakuwako na kulia na kuomboleza. Mbinguni kutakuwako na kupaza sauti na kushangilia. Kwa hiyo uko kwenye—uko kwenye mahali panyamavu sana utakapopata kuwapo, sasa hivi. Kwa hiyo afadhali upazoe, mahali pamoja ama pengine. Kwa hiyo afadhali nifanye tu chaguo langu na kwenda nyuma ya Neno la Mungu, sivyo? Niendelea tu kulisukuma kwa dhati. “Ni BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI.” Niendelea tu kusukuma. Vema.

¹⁵⁸ Naam, halikustahimili viwango vyao vya kisayansi. Na leo hii, wanapomwona Roho wa Mungu ambaye anaweza kuyatambua mawazo ya moyo, kwa kuwa Mungu alisema hivyo, kubashiri na kutabiri, kunena kwa lugha, kufasiri, karama hizi zote mbalimbali, wao wanasema, “Hiyo ni telepathia.” Mnaona? Wanajaribu kuingiza. Wao wanasema, “Vema, tunaliona likifanywa, bali mnajua kwamba ni nini, ni telepathia tu ya kibinadamu.” Lakini ni BWANA ASEMA HIVI.

¹⁵⁹ Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hivyo tu ndivyo ninavyotaka. Muda gani? “Hata ukamilifu wa dahari.”

¹⁶⁰ Haliustahimili utafiti wao wa kisayansi, kwa hiyo wanalicheka. Nao walifanya jambo lile lile katika siku za Nuhu. Loo, naam. Halistahimili hoja zao. Huwezi kulitolea hoja, bali ni Neno la Mungu vivyo hivyo. Vema.

¹⁶¹ Kwa hiyo Shetani alianza shambulizi lake juu ya kundi la Nuhu, kama tu vile alivyofanya katika Edeni. Na kila mmoja ilibidi achague, kwa imani. Utukufu! Sio kitu fulani ulichonunua, bali kwa imani. Na njia pekee unayoweza, kwa imani, kuamini uongo wa kimadhehebu, ni kulikataa Neno la Mungu, kwanza. Unawazia juu ya wokovu? *Huu* ndio. Na jinsi tu unavyoweza kutokuliamini, inakubidi kuweka imani yako katika uongo bandia wa ibilisi, kwa kutoa hoja; badala ya kuliamini Neno la Mungu, kwamba huna budi kuzaliwa mara ya pili. Na unapozaliwa, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Loo, ninalipenda hili. Hilo linasikika zuri kwangu. Unaona?

¹⁶² Amini Neno Lake, haidhuru mtu mwingine yeyote alisema nini. “Mungu alisema hivyo. Mungu alisema hivyo.”

Aseme, “Vema, Hili ni *hivi na hivi*.”

“Bali, Mungu alisema hivyo.”

“Vema, sisi, Presbiteri.”

“Sijali. Lakini, Mungu alisema hivyo.”

“Sisi ni Bap- . . .”

“Sijali. Mungu alisema hivyo.” Mnaona?

“Sisi ni Katoliki.”

“Mungu alisema hivyo.” Unaona? Dumu moja kwa moja hivi.

“Vema, mchungaji wetu ana digrii *kadhaa*.”

“Lakini, Mungu alisema hivyo.”

“Mapapa wetu wana *hili*. Maaskofu wetu wana *hili*.”

¹⁶³ “Lakini, Mungu alisema hivyo.” Kaa papo hapo. Ndiyo ngome yako, imekingwa katika Neno la Mungu, umefichwa kabisa. Jinsi ulivyo. . .

¹⁶⁴ Mbona, wewe umebatizwa katika Neno. Hiyo ni kweli. “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja, na Mwili huo ni Kristo.” Hiyo ni kweli? Naam, bwana. “Kwa Roho mmoja, sote tumebatizwa kuwa Mwili wa Mungu.” Halafu, umebatizwa katika Mungu. Umezingirwa na Mungu. Neno Lake ndilo ngome yako. Yeye ni ngome imara. “Jina la Bwana ni ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama.” Yeye ni ngome yangu, bizimu yangu, ngao yangu, viatu vyangu, kofia yangu, koti langu, moyo wangu, yote kwa yote kwangu, Mungu, yote kwa yote. Mungu! Nimefungiwa ndani Yake, nimekufa kwa ulimwengu, nikafufuka pamoja na Yeye katika ufufuo. “Siishi tena, bali ni Kristo anayeishi ndani yetu.”

Tunakutazamia kuja kwa ile siku yenye furaha
ya Utawala wa miaka elfu,
Wakati Bwana mbarikiwa atakapokuja
kumnyakua Bibi-arusi Wake anayengoja;
Loo! Ulimwengu unaugua, ukiililia siku hiyo
ya kuwekwa huru kutamu,
Wakati Mwokozi wetu atakaporudi duniani
tena. (Ndipo wenye upole watairithi dunia.)

¹⁶⁵ Kila mmoja ilimbidi kuchagua, kwa imani. Inakubidi kufanya hivyo. Wewe, siku hizi, inakubidi kuamini u—uongo wa ibilisi ama kuliamini Neno la Mungu. Hiyo ni, mojawapo. Sasa, tunaona. . .

¹⁶⁶ Hebu na tumchukue Nuhu kwa dakika moja tu, kabla hatujaondoka hapa. Ninaweza kuwazia, Nuhu, mwajua, yeye alikuwa na mambo fulani ya kupitia. Nawazia angeshuka mtaani, na kusema, “Hukumu inakuja.”

Mbona, wao, “Ni namna gani wewe. . . Ni hukumu ya namna gani?”

¹⁶⁷ “Mungu atalipiga taifa hili lenye dhambi. Wana wa Mungu wamewaoa binti za Kaini, nao hao hapo. Angalieni kile mmekuwa. Mmemwacha Mungu. Mnayo mifumo yenu mikubwa, ya dini. Mnayo mambo hayo yote, bali Mungu ataipiga dunia.”

¹⁶⁸ Kasema, “Maskini jamaa mzee, kidogo ameninii. . . Mwacheni tu. Mnaona? Yeye ni. . .”

169 Lakini yeye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Angeweza kuthibitisha yale aliyokuwa akisema, bali wao hawakuamini hilo. Mnaona? Yeye alikuwa na Neno la Bwana.

170 Sasa, labda, siku baada ya siku, nao walicheka na kudhihaki. Watoto labda walimzomea.

171 Bali Nuhu aliendelea tu kuhubiri, kwa vyovyote vile. Nayo familia yake yote na waongofu wote wakaendelea tu kuamini, kwa vyovyote vile. Wote waliokuwa wakimfuata Nuhu walimwamini Nuhu. Hiyo ni kweli. Iliwabidi kufanya chaguo lao, kuamini yale ulimwengu uliyosema, ama kuamini yale nabii huyu mwenye nguvu aliyetiwa mafuta aliyosema.

172 Kwa hiyo akasema, "Sasa angalieni. Henoko ataondoka, moja ya siku hizi, enyi kanisa. Basi akiondoka, hapo Henoko atakapoondoka, afadhali tuingie. Tutamkosa Henoko. Yeye atanyakuliwa. Kwa hiyo, afadhali tuingie." Kwa hiyo, waliangalia kwa makini wakati siku zikipita.

173 Baada ya kitambo kidogo, Mungu akasema, "Nimetosheka na kushangilia kwao. Nimetosheka na matusi yao. Nitaleta. Wachukue wanyama sasa. Panda kule juu ukapaze sauti, 'Haleluya,' mara tano hivi, nao ndege wataruka waje. Simba wote, vingine vyote, vitakuja, viwili viwili. Paza sauti, 'Bwana asifiwe,' yapata mara nne ama tano, nao hawa hapa watakuja." Mnaona?

174 Sasa, kwa hiyo Nuhu akajitayarisha. Naye... Wanyama wote wakaingia ndani, na halafu Nuhu mwenyewe akaingia. Na kwa hiyo wakati alipoingia, nadhani jambo la mwisho alilosema, alikuwa amesimama mlangoni akisema, "Ni BWANA ASEMA HIVI. Wito wa mwisho!"

175 Hapo ndipo tunaposimama leo hii, ndugu, mlangoni pa Safina. Kristo ndiye Mlango huo. Kama mtachukua hilo neno kwa neno, na mnataka kulitafakari kidogo, nendeni kwenye Ufunuo, kati ya Wakati wa Filadelfia na wa Laodikia, Yeye alisema, "Nimeweka mlango uliofunguliwa mbele zenu, nanyi mkaukataa." Mnaona? Hiyo ndiyo saa tunayoishi, kabla tu ya maangamizi. Mlango uliofunguliwa, bali wasingesikiliza. Sasa, walimtoa nje.

176 Sasa, yeye alisimama mlangoni, na kutangaza, "Saa imewadia ambapo Neno la Mungu nililonena litatimia." Hiyo ni kweli. Huyu akaingia safinani.

177 Basi alipoingia safinani, mnajua nini? Mungu aliufunga mlango. Loo, jamani! Haikumbidi mtu yeyote kuufunga. Mungu aliufunga. Hivyo tu. Nafasi ya mwisho ya kuokolewa ilikuwa imekwisha.

178 Kwa hiyo, ningewazia, watoto wakashikana mikono, kuizunguka hiyo, safina ya yapata yadi mia tano pale. Nao jamaa wazee wakatembea huku na huku na kusema, "Vema,

jamaa huyo mzee atakabwa roho hata afie mle ndani.” Mnaona? Kwa hiyo, kwenye, kumdhihaki, vivyo hivyo tu, wakimzomea. Nanyi mwajua, kila mtu. . .

¹⁷⁹ Sasa sikilizeni. Labda hili litawasaidia. Sikilizeni kwa makini. Unapolichukua Neno la Mungu, na kulifuata Neno la Mungu, kuna mara nyingi, ambapo, ukiisha kufanya yote uwezayo kufanya, imani yako inajaribiwa. Hakuna mtu hapa ila watu wa nyumbani. Nimesimama mahali hapo sasa hivi. Hiyo ni kweli. Sijui la kufanya. Uamsho umekwisha. Mnaona? Sijui wito unaofuata uko wapi. Nina ninii tu—ninasimama tu, nikiangalia kwa wasiwasi, nikishangaa ni nini kinachofuata.

¹⁸⁰ Nuhu aliingia. Aliyafuata mapenzi ya Mungu. Mungu akaufunga mlango nyuma yake, bali haikunyesha kwa siku saba zaidi. Unashangaa Nuhu aliwazia nini, wakati huo wote mle ndani? Huku Nuhu ameketi safinani, mlango umefungwa. Akawaza, “Wakati wowote tu, enyi watoto, mtaisikia. Tutauvuta mlango, hiki kifuniko hapa juu.” Walikuwa juu kwenye orofa ya juu, mwajua. Wanyama kwenye ya chini, ndege kwenye hiyo inayofuata, nao walikuwa juu. Hilo jua. . . “Loo, asubuhi, kutakuwa—kutakuwa na kitu huko, kuingia giza, mvua itakuja.” Lakini, kesho yake asubuhi, jua likachomoza.

¹⁸¹ Labda watu wengine, ambao kidogo walimwamini Nuhu nusu nusu, huenda walikwea kule na kusimama kuizunguka safina, kasema, “Mnajua nini? Mzee huyo huenda alikuwa sahihi. Afadhali tusimame hapa.” Vema, ndipo “wakaona kosa.”

Manabii wa Mungu hawafanyi kosa lolote. Neno la Mungu haliwezi kushindwa.

¹⁸² Mlinisikia nikihubiri juu ya, kuhusu Yona akishuka kwenda Ninawi. Wao walisema alikuwa amerudi nyuma. Hakika hakurudi nyuma. Alikuwa moja kwa moja katika mapenzi ya Mungu. Kweli kabisa. Alikuwa na Neno la Bwana, naye akatembea ndani Yake.

¹⁸³ Hapa, Nuhu akasema “Sasa, enyi watoto, ninyi nyote karibieni hapa, nanyi mtaona wingu la kwanza lililopata kuja angani. Litapanda juu, asubuhi.” Vema, jua likachomoza. “Vema, labda kufikia saa tatu. Tutaangalia kwenye saa tatu. Saa nne? Saa tano? Saa sita? Saa tisa? Saa kumi? Kumi na moja? Thenashara? Whiu! Yeye aliufunga mlango jana, pia.”

¹⁸⁴ Baadhi yao wakasema, “Vema, mnajua nini? Nitakubaliana na Dada Susie huko chini kwenye ninii lile kuu. . . katika kanisa lake kuu. Mzee yule ana kichaa. Mnaona? Alipanda kule na kufunga ule mlango, na kusema, ‘Mvua itanyesha,’ naye yule pale ameketi. Halafu, basi, hakuna kitu kwake. Mnaona? Jua lilichomoza moja kwa moja, likaenda ng’ambo ya pili kama lifanyavyo sikuzote. Hakuna kitu kama mvua.” Kwa hiyo, waaminio nusu nusu, vuguvugu, shingo upande, ambao hawako

tayari kumchukua Mungu, moja kwa moja hata mwisho wa safari, waishi au wafe! Mnaona ninalomaanisha?

¹⁸⁵ Simama katika hali yako ya kuzungushiwa ngome. Uishi ufe, utumbukie uzame, kaa pale pale vile vile tu.

¹⁸⁶ Wakati Ibrahimu, baba wa waaminifu, alipokichomoa kile kisu, akazivuta nywele nyuma ya kichwa cha mwanawe, apate kulikata koo lake, yeye alisema, “Nimeshawishika ya kwamba Mungu anaweza kumfufua katika wafu, katika umbo ninalomhisia.” Alikuwa tayari kulifuata Neno la Mungu hadi mwisho. Mnalipata?

¹⁸⁷ Haijalishi ni nini, dumu moja kwa moja hapo. Kama kila kitu kinaonekana kuwa, huwezi kwenda inchi moja mbele zaidi, nenda hiyo inchi. Na kama ukigonga ukuta, simama hapo mpaka Mungu afanye njia ya kupitia.

¹⁸⁸ Siku ya kwanza ilipita, siku ya pili ikapita, siku ya tatu ikapita, nne, tano, sita. Mwajua, Nuhu alikuwa na mengi sana ya kufanya. Ninawazia baadhi ya kusanyiko lake walisema, “Baba, unafikiri kwamba tunapaswa kupanda tutokee dirishani? Unafikiri yote yalikuwa ni kosa?”

¹⁸⁹ Akasema, “La, la, la. Ni nani Yule aliyemtwa Henoko? Ni nani Yule aliyefunga mlango huo? Ni nani Huyo aliyefanya mambo hayo yote mbele zetu? Kama Yeye ametuongoza umbali huu, na kutufungia ndani, hebu na tukae pamoja Naye.”

¹⁹⁰ Jambo ndilo hilo, Kanisa. Kama Yeye ametuinua kutoka ulimwenguni, na kutuongoza umbali huu, na kutufungia ndani pamoja na Yeye, huku Roho Mtakatifu ametuzunguka kote, ndani yetu, na kupitia kwetu, hebu na tumfuate kote. Hiyo ni kweli. Wakati huo utakuja. Wakati utakuja. Acheni wenye kudhihaki waseme watakalo.

¹⁹¹ Ndipo, kwenye siku ya saba, asubuhi hiyo watu walikuwa nje barabarani. Hawakuwa wameona kitu kama hicho. Mawingu yalikuwa yanatanda, ngurumo kuu za radi, radi ikimulika kote angani. Yapata saa moja, matone makubwa mno ya mvua yakaanza kuanguka, kwa mara ya kwanza, kwenye uso wa nchi. Nawazia ndege walikuwa wakilia. Kila umbile lilirauliwa kabisa. Wanadamu wakaanza kushangaa, na kusema, “Toeni vifaa vyenu vya kisayansi. Ijaribuni rada yenu. Twambieni. Haya yote yanahusu nini?” Bali isingefanya kazi. “Hatujawahi kuona kitu kama hicho maishani mwetu mwote.” Vema, yapata adhuhuri, vijito vilikuwa vimeanza kujaa. Yapata kesho yake asubuhi, mito, vilindi vilikuwa vimepasuka.

¹⁹² Yapata siku za kwanza tatu ama nne, maji yalikuwa yamejaa kote mitaani, gharika. Watu walikuwa wakija karibu na safina, wakipiga mlango. “Fungua!”

¹⁹³ Nuhu alikuwa akiabiri moja kwa moja juu ya mawimbi. Yakafikia yapata futi ishirini na kitu, ninaamini Biblia ilisema, safina ikainuka ku—kutoka ardhini, ikaanza kuelea ikipembea.

¹⁹⁴ Wakapanda kilele kilichokuwa kirefu zaidi, wakaning'inia kwenye tawi lililokuwa juu kuliko yote. Wakapiga mayowe. Na kila kitu kilichokuwa na pua za kupumulia, kikaangamia, ambacho hakikuwa ndani ya safina hiyo. Kila kitu kilichopumua kikafa. Wangeweza kulia wapate rehema, wangeweza kulia, bali walikuwa wamemkataa Mungu kwa dharau mara nyingi sana mpaka hakuna kitu cha kufanya ila kuleta haki Yake. Nayo haki Yake ilikuwa ni hukumu.

¹⁹⁵ Kama vile alivyomwambia Hawa, “Siku utakapokula kutoka kwake, siku hiyo utakufa.”

¹⁹⁶ Sasa, ninawatakeni muone. Tumeona. Tumeona sasa, mara mbili, ambapo Neno liliingia katika mapambano na hoja. Na sasa yamerudi tena, hoja dhidi ya Neno. Sasa unaweza kuchagua.

¹⁹⁷ Yoshua alisema jambo lile lile. Yeye alisema, “Sasa, kama mkitaka kuchagua kuitumikia miungu baba zenu waliyoitumikia kabla ya gharika, mnaona, ama mchague kuitumikia miungu ya Waamori ambao mmeikalia nchi yao? Baba zao kabla ya gharika, walielea wakapita mafuriko, walioliamini Neno la Mungu. Waamori walilikataa Hilo. Mungu amewapa nchi yao. Sasa, kama mnafikiri ni vibaya kumtumikia Mungu, chagueni leo hii yule mtakayemtumikia. Lakini kwangu mimi na nyumba yangu tutadumu moja kwa moja na Bwana.” Amina. Ninapenda hilo. Mapambano.

¹⁹⁸ Angalieni. Ile siku ambayo ile ngome ilivunjwa, katika Edeni, mwanadamu alitoka “nje.” Amina. Walitoka nje. Nayo ile siku waliyoweka agano la Mungu, kwenye yale maangamizi yaliyotangulia gharika, waliingia “ndani.” Walitoka Edeni. Wakaingia ndani ya safina. Na kwenye hii ya tatu, watapaa “juu.” Kutoka, kuingia, kupaa juu! Amina. Tunaona yale waliyofanya mara mbili. Nitasimama pamoja na Bwana. Hivi hamtaki kusimama? Ninataka kulitimiza Neno la Mungu.

¹⁹⁹ Yesu alisema, “Kama siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Kweli dhidi ya uongo; Nuru dhidi ya giza; Uzima dhidi ya mauti; Neno dhidi ya sayansi. Hiyo ni kweli. Utafiti wa sayansi utakanusha Neno, kama wanavyofikiri unalikanusha, bali haulikanushi Neno.

²⁰⁰ Shetani alikuwa, anao mfumo wake ukifanya kazi tena, kuwafanya watu wasiliamini Neno la Mungu. Njia mbaya ya Shetani ya kuabudia, kama vile Kaini na kama Baalamu, wao ni wa kidini sana.

²⁰¹ Kaini alikuwa ni wa kidini. Alileta madhabahu, akafanya madhabahu. Na, kwa kweli, Kaini alikuwa ni wa kidini kuliko Habili. Ndivyo hakika. Alimfanya Bwana mengi kuliko Habili

aliyofanya, bali Habili alikuja kwa njia ya Neno. Hivyo tu. Alifanya mengi zaidi. Alijenga dhehebu kubwa. Alijenga kitu kikubwa, urithi mkubwa wa Ukristo. Lakini, mnaona, yeye alikuja kwa njia mbaya. Naye alikuwa . . . Haikukubalika. Sasa, mbaya, kwa kuwa ilikuwa ni kinyume na Neno.

²⁰² Balaamu alikuwa ni wa kidini tu kama Musa. Alikuwa pamoja na dhabihu ile ile, wana-kondoo wale wale, wanyama wale wale safi, na kila kitu. Na kumwomba Mungu yule yule, na kutoa dhabihu kwa Mungu yule yule ambaye Musa alimtolea, ingawa alikuja kwa njia mbaya. Mnaona? Ilikuwa ni kinyume na Neno, kama ilivyokuwa huko Edeni.

²⁰³ Neno halitachanganyana na nadharia ya kisasa. Mnaona? Huwezi kuwa na nadharia ya kisasa. Sasa, katika kufunga, sikilizeni kwa makini. Neno halitachanganyana na nadharia yoyote ya kisasa. Haliwezi kuwa na nadharia na liwe na Neno. Inakupasa kuwa na Neno ama nadharia. Sasa utaamini gani?

²⁰⁴ Kama Biblia inafundisha ubatizo ni “katika Jina la Yesu Kristo,” nalo kanisa linasema ni “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” basi utaamini nani? Kama Yesu alisema, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili,” nalo kanisa linasema, “Njoo ukajiunge,” sasa utaamini nini? Kama Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” nalo kanisa linasema “wewe ni mfuasi mzuri tu,” utamwamini nani? Kama Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo mimi nyinyi nanyi mtazifanya,” nalo kanisa linasema “siku za miujiza zimepita,” utamwamini nani?

²⁰⁵ Mnaona ninalomaanisha? Ningeweza kusimama hapa saa moja, moja kwa moja kupitia mambo hayo, nikiyaleta hayo mambo mbalimbali, jinsi ambavyo nadharia imejenga mfumo wa kulipinga Neno la Mungu.

Sasa, enyi Wakristo, kaeni nyuma ya Neno. Naam, bwana.

²⁰⁶ Njia mbaya ya maisha, kujaribu kulichanganya. Leo hii wanawachukua wanawake hawa waliovalia vyovyote vile. Wanawachukua wanaume hawa, kama wanavuta sigara, kunywa pombe, ama kitu kingine chochote, wanawafanya mashemasi, na kadhalika, kanisani, hata wachungaji. Hawa waliovalia, wanawake, vyovyote wanavyotaka kuvalia, na kuwaingiza ndani na kuwafanya dada kanisani. Kamwe usijaribu kuingia Mbinguni namna hiyo. Kamwe haitachangamana na nadharia ya kisasa.

²⁰⁷ Kwa hiyo, tunayo matabaka mawili siku hizi yanayokiri. Sasa sikilizeni kwa makini, katika kufunga. Tunayo matabaka mawili yanayokiri kuwa Bibi-arusi wa Kristo. Hiyo ni kweli. Nayo Biblia inasema kutakuwako na matabaka mawili. Hiyo ni kweli. Wanawali wenye busara na wale wapumbavu. Hiyo ni kweli? Kunayo matabaka mawili.

²⁰⁸ Kanisa linasema, “Sisi ndio Kanisa.” Wanatoka wanaenda kufanya miamsho hii mikubwa ya kiinjalisti, wanawaleta watu

kanisani. Wanawake wanaendelea na njia yao ya kufanya. Wanaume wanaendelea na njia yao ya kufanya.

²⁰⁹ Kamwe hawabadilishi fundisho lao. Wameliandika lote, na kuliweka kwenye hati, na kulikaza, na hizo Kanuni ya Imani ya Mitume, na sala fulani, na katekismo hizi zote, na kila kitu ambacho Wamethodisti, na Wabaptisti, na Wapresbiteri, na Katoliki, na wote hao, wanachosoma. Nao wanaikubali hiyo katekismo kwa sababu baadhi ya watu mashuhuri huko nyuma walisema hiyo ilikuwa ni sawa. Huenda alikuwa ni mtu mashuhuri, huenda alikuwa sahihi, bali hana mamlaka ya kusema hivyo.

²¹⁰ Maana, Biblia ndiyo mamlaka ya Mungu. Ni Neno la Mungu lililoandikwa. “Na mtu yeyote atakayeongeza jambo moja Kwake, au kuondoa lolote kutoka Kwake, huyo ataondolewa (sehemu yake) kutoka kwenye Kitabu cha Uzima.” Hilo haliwezi kufanywa hivyo, sasa.

²¹¹ Lakini tunao wawili wanaolikiri hilo. Mmoja alisema, “Vema, sisi ndio Kanisa.” Huyo mwingine akasema, “Sisi ndio Kanisa.” Vema.

²¹² Wenye hekima na wapumbavu, wote wawili wamealikwa. Bali mliona? Wote wawili walikuwa na vyombo. Hiyo ni kweli. Wote wawili walikuwa ni bikira, waaminio. Wote wawili walikuwa na vyombo.

²¹³ Lakini, Shetani ana uwezo kuliko wetu. Tunajua hilo. Tunajua ya kwamba Shetani ana uwezo mwingi mno ku—kuliko mwanadamu yeyote. Kamwe usijaribu kufanya hivyo kwa hekima yako, kumshinda akili. Huwezi kabisa kumshinda.

²¹⁴ Yesu alijua jambo hili, kwa hiyo Yeye alituma Kanisani, kwamba, kusudi Shetani asiwashinde akili, mahali pa kujihami. Yeye aliwatumia Roho Mtakatifu. Nalo Kanisa halidai kuwa jerevu. Wanadai tu kuamini.

²¹⁵ Wahubiri wao hawawezi kutoka na kuwaonyesha Ph., L. maradufu, Q.U., S.T.D. zao, na mambo haya mengine yote. Hawana nyakati kuu, kubwa za kuzinduliwa wakati wanapowekwa katika shirika fulani la wahudumu. Mwajua, nilizoea kuimba wimbo fulani mdogo:

Hawa watu huenda wasijifunze kuwa,
Wala kujivunia umaarufu wa kilimwengu,
Wote wamepokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
Nao wanatangaza sasa karibu na mbali pia,
Nguvu Zake zingali ni zile zile,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao.

²¹⁶ Naam, bwana. Naam. Hawana mambo haya makubwa. Hawadai kujua chochote. Wanadai tu kuamini kitu Fulani.

217 Yesu alimtuma Roho Mtakatifu, ambaye ni Yeye Mwenyewe. Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa ndani yenu; nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.”

218 Sasa, sasa, sasa angalieni. Yesu alijua hilo, kwa hiyo akamtuma Roho Mtakatifu kulithibitisha Neno. Whiu! Mlilipata? Mnaona? “Kuthibitisha,” kwa wale waliojihami nyuma ya Neno, “kwamba Yeye yuko katika Neno.” Mnaona?

219 Waache huko nje. Wataucheka huo mfumo. Wanasema, “Wao wana kichaa.”

220 Lakini Yesu alimtuma Roho Mtakatifu, ambaye ni Yeye Mwenyewe, kuwafikishia wale walio nyuma ya Neno, kama kundi la Ibrahimu, kulithibitisha Neno mbele yao, kuonyesha ya kwamba Yeye angali ni Neno. Kuona kwamba umepachukua mahali pazuri! Vema.

221 Moto ni thibitisho la Nuru ikitoka kwenye Neno. Watajaza... Yule bikira mwerevu, mwanamwali mwenye busara, alikuwa na Mafuta katika taa Yake, na Yeye aliitengeneza taa Yake na kuiwasha. Sasa, ni kitu gani? Sasa ninii... Mungu ni Neno. Mafuta ni Roho. Nao Moto ni Nuru ya Injili juu ya Mafuta hayo. Mungu alisema hivyo. Mnaona? Hicho ndicho chombo. Vema. Mafuta yako kwenye chombo. Nao Moto, ukiyawasha, inaonyesha kwamba unaakisi ile Nuru ya kile Neno lilichosema. Mnaona? Huo ndio uakisi. Sasa, huyo mwanamwali mwenye busara angeweza kufanya hivyo.

222 Lakini huyo mwingine, mwanamwali mpumbavu, alikuwa nje, hakuwa na Mafuta, wala wasingeweza kuakisi chochote ila kanisa lao tu na dhehebu lao. Mnaona?

223 Sasa, wewe unasema, “Neno, ulisema ‘Neno lilikuwa—lilikuwa Roho?’” Naam, bwana.

224 Mungu alisema, “Neno langu ni Roho.” Hiyo ni kweli. Bibi-arusi wa kweli hana budi kuunganishwa na Neno. Sasa, kumbuka, ikiwa Yeye ni sehemu ya Kristo, Yeye hana budi kuwa Neno la Kristo. Kusudi uwe Neno la Kristo, huna budi kubatizwa katika Kristo. Basi unapokuwa ndani ya Kristo, unamwamini Kristo, naye Kristo ni Neno.

Amina! Amina! Amina!

Unaamini Hilo? Amina!

Mnampenda? Amina.

Mtamtumikia? Amina!

Amina! Amina!

Yeye ni Nuru ya ulimwengu. (Hiyo ni kweli.)

Amen!

Yeye ndiye furaha ya moyo wetu. Amen!

Yeye ndiye Nguvu za maisha yetu. Amen!

Amen! Amen!

225 Bi—Bibi-arusi hana budi kuunganishwa, kuunganishwa pamoja na Neno. “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.” Nayo *Hii* ndiyo Sauti Yake kwenye Neno lililoandikwa. Vema. Lililounganishwa kwa Neno, Yeye anajiweka tayari, sio kwa kanuni ya imani ya kawaida.

226 Kama vile Esta, wakati Esta alipokuwa achaguliwe kusimama mbele ya mfalme, hakujipamba kwa vitu vyote, bali alijipamba kwa roho mtamu, mpole. Hicho ndicho Bibi-arusi anachojivika nacho, huku matunda yote ya Roho yakimfuata.

227 Ana nini? Anakusanyika pamoja katika ushirika wa Neno.

“Amina.”

228 Ushirika wa Neno. Hiyo ni kweli. Kushiriki, kuketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, usiku wa leo: moyo mmoja, mahali pamoja, Roho mmoja, nia moja, tumaini moja, Mungu mmoja, kusudi moja. “Amina.” Mnaona? Haya basi. Kila wakati Biblia inaposema jambo lolote, tunasema, “Amina.” Kuliitikia kila Neno kwa “Amina.”

“Yesu Kristo, yeye yule jana, na hata milele.”

“Amina!”

“Tubuni, mkabatizwe, Jina la Yesu Kristo.”

229 “Amina!” Mnaona, kila kitu, “Amina! Amina! Amina!” tu, moja kwa moja kuendelea, mnaona, katika ushirika.

230 “Matunda ya Roho.” Yake, Yeye ana nini? Tunda la Roho ni nini? Furaha, furaha ya moyo Wake, kujua kwamba Yeye anakuja karibuni. “Amina, na Amina! Amina!” Naam.

231 Utulivu wa moyoni. Kwa nini? Utulivu wa moyoni. Utulivu wa moyoni. Mwajua nini? Haijalishi kijacho wala kiendacho, acha meli iyumbeyumbe, acha dhoruba zije, acha radi imulike, ngurumo zingurume, chochote kinachotukia, haileti tofauti yoyote. Mabomu ya atomiki yanaweza kuanguka. Mnaweza kujenga ngome za miamba, ngome za bomu, chochote mtakacho, bali Yeye angali anasema, “Amina! Amina! Amina!”

232 Kwa nini? Yeye amelindwa ndani ya ngome. Ati nini? Amelindwa ndani ya nini? Neno, Neno (nini?) lililofanyika mwili, likikaa miongoni mwetu, tukimwangalia Yeye akitenda kazi miongoni mwetu, katika kusanyiko letu. Mnaona? Huyu hapo. Kwa hiyo inaleta tofauti gani? “Amina!” Acha mapambano yaendele.

Nimetia nanga nafsi yangu katika mahali pa
raha,

Nisiabiri bahari zenye tufani tena;

Tufani zaweza kupitia juu ya vilindi vyenye
dhoruba,

Lakini katika Yesu mimi ni salama milele.

233 Unasema uko ndani ya Yesu halafu ulikane Neno Lake? Kuna kasoro fulani. Yeye daima husema “amina” kwa Neno Lake Mwenyewe. Mnajua hilo. Kweli. Vema.

234 Kukusanyika kwa ajili ya ushirika. Furaha, moja ya matunda ya Roho. Utulivu wa moyoni. Na imani katika Neno. Amani, furaha, imani, uvumilivu, saburi, utu wema.

235 Imani, imani ya namna gani? Unaitumia imani yako kwa njia gani, kuyapiga mapambano? Utaitumia imani yako kwenye nadharia fulani, juu ya hoja fulani, jambo fulani? “Si ni jambo la maana kwamba karibu watu wote huja kwenye kanisa hili? Hili si ni kanisa kubwa?” La, bwana, sivyo. Ikiwa kanisa hilo halihubiri kila Neno la Biblia hiyo hapo, na “amina” kwa kila Neno Lake, linaamini kila ishara, kila ajabu, na kuziona zikitenda kazi moja kwa moja miongoni mwao, ningeliondokea, haidhuru ni kubwa jinsi gani, ni dogo jinsi gani. Mnaona?

236 Imani, upendo, furaha, amani, na imani katika Neno. Kwa hiyo acheni Shetani alenge bunduki zake. Tumetia nanga. Amina. Hatudai kuwa watu mashuhuri. Sisi si watu mashuhuri, machoni pa ulimwengu. Sisi ni watu wanyenyekevu, wakulima wadogo. Hatuuajali utajiri wa ulimwengu.

237 Rafiki yangu, usiku wa leo, nilianza kuihubiri Injili hii. . . Inachelewa, kwa hiyo nitaondoka, angalia, kwa ajili ya usiku wa leo. Tulianza kuhubiri yapata miaka thelathini, kitu fulani, ama miaka thelathini na mmoja iliyopita. Yapata mwaka wa 1930, '31, mahali fulani hapo, nilianza kuhubiri Injili. Nimehubiri Ujumbe uu huu, na kamwe sijabadilisha kutoka kwa Huo, kwa kuwa ni Kweli. Nimedumu tu moja kwa moja na Huo.

238 Sasa, usiku wa leo, mimi ni mtu wa makamu, umri wa miaka hamsini na mitatu, babu. Nampenda kuliko nilivyompenda huko nyuma, kwa sababu nimemwona Yeye katika majaribu zaidi na vita. Nami nimeona, nilipofikia mahali ambapo palikuwa na majaribu mengi sana, niliposema jambo fulani, kama vile Nuhu katika safina, “Hili litakuwa.”

“Sasa, angalieni. Loo, rehema! Mungu, nini. . .”

239 “Itakuwa.” Kaa hapo. “Itakuwa.” Jua linapita. “Itakuwa.”
“Wajuaje, Ndugu Branham?”

240 “Mungu alisema hivyo. Itakuwa. Haina budi kuwa. Mungu alisema hivyo.” Kwa hiyo, nimetia nanga nafsi yangu katika Mahali pa raha. Katika Yesu mimi ni salama milele. Hata nini lije ama liende, hebu tulichukue kwa njia hiyo.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, kumpa Yeye shukrani.

241 Kunaye mtu hapa usiku wa leo, ambaye hamjui Yeye wala hajatia nanga jinsi hiyo? Hujachukua msimamo wako mkuu pamoja na Neno la Mungu, nawe ungesema, “Ndugu Branham, nitainua mkono wangu, na kusema, ‘Unikumbuke katika maombi.’ Sijawahi kuchukua msimamo kama huo,

kwamba ningemtumaini Mungu haijalishi kile kitakachotukia. Ningelichukua Neno Lake, bila kujali kile mtu yeyote alisema ama kufanya, ningali niliamini Neno Lake. Ninataka uniombesha, Ndugu Branham. Ninaamini mapambano yanaendelea, nami nimechukua msimamo wangu katika...Sijawahi kuchukua msimamo wangu, bado. Ninataka kuuchukua, upande wa Mungu, na pamoja na Neno.”

²⁴² Ni wangapi, basi, tayari mmechukua msimamo wenu, na mnasimama nyuma ya Neno la Mungu? Inua mkono wako, useme, “Nina shukrani sana kwamba niliuchukua.” Mungu akubariki. Asilimia mia moja. Mungu apewe sifa, hata watoto wadogo wanainua mkono wao. Jamani, jamani!

²⁴³ Loo, kama hili si halisi! Mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tumelindwa kwa Neno. Tumelindwa kwa Neno, pamoja na Uwepo wa Roho hapa, akithibitisha, kutuhakikishia, kama walivyofanya katika siku za mwanzoni: Injili ile ile, ishara zile zile, maajabu yale yale, Mungu yule yule, Neno lile lile, kuyafanya mambo yale yale yatimie.

²⁴⁴ Watu wakisimama, Roho akishuka juu ya watu pamoja na karama ya unabii, unabii mwingi. Mmoja atasimama, Roho awashukie, kunena kwa lugha. Watanena kwa lugha, watulie, na mwingine ataufasiri; nao utatimia. Loo, jamani!

²⁴⁵ Tukiona nguvu zetu kuu za Roho Mtakatifu zikiyabadilisha maisha yetu kutoka kwa maisha ya dhambi, kututoa humo, na kutufanya viumbe vipya katika Kristo Yesu. Jinsi tunavyomshukuru Bwana!

²⁴⁶ Baba wa Mbinguni, ni vema sana kukusanyika pamoja na kundi hili la watoto Wako, usiku wa leo, hawa wanaokaa hapa chini Clarksville kwa muda. Furaha sana kuliona kanisa hili likisonga mbele, kumwona mchungaji, hakuna asiyeamini hata mmoja miongoni mwa watu, wote katika Kimbilio. Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa hilo, Baba!

²⁴⁷ Ninawazia juu ya paa mdogo, wakati mmoja. Alikuwa ametoka kwenye kimbilio, nao mbwa wakubwa walikuwa wakimfuata. Naye alikuwa akikimbia ayaokoe maisha yake. Basi alipofikia kwenye ua ambapo kimbilio lilikuwa, alirukia uani, naye akafurahi sana. Akakoroma, kisha akageuka na kuwaangalia hao mbwa, maana alikuwa salama. Wasingeweza kuupanda huo ua, hawakuumbwa hivyo. Kama wangeugusa huo ua, wangepigwa na mshtuo wa umeme.

²⁴⁸ Hivyo ndivyo tulivyo, Bwana. Tunapoenda nyuma ya huo—huo Ua wa Neno la Mungu, Nguvu za umeme za Roho Mtakatifu humzuia adui wetu. Yeye hawezi kuuruka huo Ua; hajaumbwa hivyo. Baba, tunakushukuru kwamba Wewe umetufanya hivi kwamba tungeweza kuruka tupate usalama, Bwana, ndani ya Kristo Yesu. Tuna furaha sana, Bwana, salama daima.

249 Tunaomba sasa kwamba utalibariki kanisa hili dogo, mchungaji wake, wapendwa wake. Bariiki wote walio hapa, usiku wa leo. Mbariki kila mhudumu.

250 Tunamwombea Ndugu yetu Neville wa thamani na muungwana sana. Na sasa, kama jana, Shetani angejaribu kumvuta atoke jukwaani, akimongesha kwenye hilo gari. Naye angejaribu kufanya jambo baya, bali Wewe ulikuwa pale jukwaani. Mungu, yeye alijaribu kunichukua hivi majuzi, huko mahali pa kulenga shabaha kwa bunduki, bali Wewe ulikuwa pale jukwaani. Alijaribu kumchukua Ndugu Willard Crase, wakati alipoigonga ile nguzo, bali Wewe ulikuwa hapo jukwaani. Loo, ni vema sana kukujua Wewe. Kama vile mshairi alivyosema wakati mmoja:

Ni tamu sana kumtumaini Yesu,
Kuliamini tu Neno Lake,
Kutulia tu juu ya ahadi,
Kujua tu, "BWANA ASEMA HIVI."

251 Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya hili! Bariiki nafsi zetu. Samehe dhambi zetu. Yaponye maradhi, Bwana, yanayokaa miongoni mwetu. Tunajua ya kwamba maskini miili hii ipatikanayo na mauti ni minyonge, nayo inayumbayumba chini ya athari ya maradhi, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utatuweka vema, tupate kuihubiri Injili. Jalia tuishi miaka mingi yenye furaha kama Yesu akikawia.

252 Na jalia sote tuwe tayari kwa ajili ya Unyakuo, sote katika Safina ya usalama, ndani ya Kristo Yesu, kwa Roho mmoja, tumebatizwa mle; huko juu kwenye orofa ya juu, ambako tunaweza kuiona Nuru ya Injili ikimulika ndani, na kuitikia kila Neno kwa "amina." Tujalie, Bwana. Wabariki na uwahifadhi. Ninawadai kwa ajili ya lulu za taji Yako, Bwana, katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

253 Sasa, kama tujuavyo, Neno wakati mwingine hukata, bali tunalipenda hivyo. "Neno la Mungu," ilisema Waebrania 4, "ni kali kuliko upanga ukatao kuwili." Hukatilia mbali kila kitu, makali kuwili, kuja na kwenda. "Tena lina nguvu zaidi pia, jepesi zaidi, likikata hata kutenganisha, kwenye mafuta ya mfupa, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Ni kitu gani? Neno! Neno! Mnaona? Na sasa, tukiisha kuwa na Ujumbe mgumu, unaokata kwelikweli, mliufurahia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana. Mapambano! Hivi hamna furaha mmelindwa ngomeni, usiku wa leo? ["Amina."] Linajenga imani na nguvu na tumaini, kwa Kanisa. Loo!

Juu ya Kristo Mwamba wenye imara
nasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

254 Sasa hebu tumwabudu tu Yeye kwa yapata dakika mbili ama tatu, sivyo? Hebu na tufunge tu macho yetu, tuinue mikono yetu.

255 Dada, mpendwa, tupe sauti, *Nampenda*. Sivyo, juu ya huo? Nitaipata.

Nampenda . . .

Jiachilieni tu sasa. Abuduni!

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

256 Sasa hebu tuangaliane, na kupeana mikono mmoja kwa mwingine. Tuseme:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

257 Kalvari ilikuwa ni nini? Kadeshi-barnea Yake. Yeye alifanya nini? Alipanda kule, na kusema, “Mwanadamu ataishi baada ya kifo. Nitawathibitishieni.” Akapanda kule, hata Kadeshi-barnea, akaichukua hukumu yetu sote. Kalvari! Akafa kwa ajili ya dhambi zetu, kisha akauvuka mto wa mauti. Katika siku hiyo ya tatu, akarudi. Lile jiwe likabingirika chini ya kilima, na Yeye akatoka, hai.

Baadhi yao walisema, “Yeye ni roho.”

258 Kasema, “Niguseni. Hivi roho ina nyama na mifupa kama nilivyo nayo?” Kasema, “Mna chakula chochote?”

259 Wakasema, “Tuna mkate wa asali hapa chini, nadhani, na samaki.”

260 Kasema, “Hebu tupate kipande chake.” Nao wakachukua wakala. Akasema, “Mnaona, pepo hali kama ninavyokula.” Yeye akasema, “Sasa, nyinyi nendeni huko Yerusalemu, mkaanze na Injili, kutoka huko. Nami nitawatumieni Malimbuko ya . . . ya kufufuka kwenu, maana nitawainua kutoka kutokuamini kwa Neno, na kuwafanya mwe na imani katika Hili, na kuamini. Nanyi mtakuwa juu ya dhambi na kutokuamini kwote. Na hivyo, wengine wataanguka katika zamu ya kwanza, zamu ya pili . . .”

261 Kumbukeni, hao . . . Zamu ya saba, mlikumbuka hilo? Zamu ya saba ndipo Yeye ajapo. Zamu ya saba ilikuwa ni nini? Ujumbe wa Malaika wa saba. Zamu ya kwanza, wao walilala usingizi, zamu ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita; kotekote, Thiatira, na kotekote kupitia nyakati zote, kufikia zamu ya Laodikia. Lakini kwenye zamu ya saba, Sauti ikaja, “Haya, Bwana-arusi

yuaaja, tokeni mwende kumlaki.” Na kitu gani? Waliamka na kuzitengeneza taa zao.

Nampenda, nampenda
Kwani . . .

262 Mko kwenye mwisho?

. . . Yeye kwanza . . .

[Mtu fulani anamwambia Ndugu Branham, “Nina kanda yapata kiasi *hicho*.”—Mh.]

Basi . . .

263 Waweza kuupata? Una kiasi *hicho* kilichosalia? Una kiasi *hicho* zaidi cha kanda? Uko karibu kumaliza? Kanda karibu imekwisha? Endelea, endelea.

Mtini Kalvari.

264 Loo, jamani! Dada Ruth, sikumaanisha kuizima. Nilifikiri nilikuwa nikijaribu kucheza nyimbo hizi nzuri. Nilitaka huo urekodiwe, unaona. Nilikuwa nikijaribu kufanya, kuzishika nyimbo hizi, unaona, wakati zikiendelea. Hivi hamuupendi huo?

265 Mwajua, ninapenda uimbaji mzuri, wa kale wa kipentekoste, ila sikuzote nilisema nachukia sauti iliyofunzwa kupindukia, wale watakaoishikilia pumzi yao mpaka wamekuwa samawati usoni, wengine, “*Kuvuruta sauti!*” Nao hawaninii . . . hawaimbi, wanapiga tu kelele. Mnaona?

266 Napenda uimbaji ule mzuri, wa kale, mwajua, unaotoka moyoni mwako, kama—kama:

Amina! Amina! Amina!

Nanyi je? Ninaupenda huu.

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni
Mmoja;

Pepo watatetemeka, na wenye dhambi
wataamka;
Imani katika Yehova hufanya chochote
kitikisike.

267 Amina. Huufanya ufalme huu wa ibilisi uporomoke na kuanguka. Kuyageuza hayo maneno makubwa ya kulipusha juu ya, “BWANA ASEMA HIVI.” Neno hilo la Mungu la atomiki linaruka huko nje na kuuvunjavunja ufalme wa Shetani. Amina. Ndipo, “Twendeni askari Wakristo, tukienda taratibu kama vitani.” Hiyo ni kweli. Vema.

268 Hebu tuimbe tena sasa, kila mtu, kwa sauti yako yote, huku macho yenu yamefungwa, mikono juu hewani, *Nampenda*. Vema, dada, kipenzi. Vema.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁶⁹ Baba wa Mbinguni, katika mikono Yako sasa tunauweka utu we—wetu. Fanya nasi upendavyo. Tunatumaini Wewe utatutumia, Bwana, kuileta Nuru kwa wengine katika jamii yetu na popote tutakapoongozwa. Na, Mungu, utuangalie sasa, na kutulinda hata tutakapokutanika tena, na kuleta miganda ya thamani. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

²⁷⁰ Sasa, ni furaha kuwa pamoja nanyi nyote, usiku wa leo, kuwa na wakati wa ushirika. Nitairudisha mimbara kwa mchungaji wenu mpendwa, Ndugu Junie.

Vema, Ndugu Junie. 

62-0531 Mapambano Kati Ya Mungu Na Shetani
Faith Assembly
Clarksville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org